# NAFASI YA VIJANA KATIKA RIWAYA ZA

# *PENDO LA KARAHA* NA *KOVU MOYONI*

**NA**

**KIHARA ISAAC SIMON**

**C50 / 68609 / 2013**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2016**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo Kikuu kingine.

……………………………………… ……………………………………

**Kihara Isaac Simon** Tarehe

**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

……………………………………… ……………………………………

**Prof. Mwenda Mbatiah** Tarehe

**(Msimamizi)**

……………………………………… ……………………………………

**Dkt. Evans M. Mbuthia** Tarehe

**(Msimamizi)**

# YALIYOMO


Ungamo ..................................................................................................... ii

Kutabaruku ................................................................................................ vi

Shukrani .................................................................................................... vii

Ikisiri ......................................................................................................... ix

**SURA YA KWANZA**

1. 1 Usuli wa Mada ......................................................................................... 1

1. 2 Tatizo la Utafiti ........................................................................................ 2

1 . 3 Malengo ya Utafiti .................................................................................. 3

1. 4 Maswali ya Utafiti ..................................................................................... 3

1. 5 Sababu za kuchagua mada ......................................................................... 3

1. 6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ......................................................................... 4

1. 7 Msingi wa Nadharia .................................................................................. 4

1. 8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ..................................................................... 6

1. 9 Mbinu za Utafiti ........................................................................................ 9

**SURA YA PILI**

**TATHMINI YA HALI YA JAMII KATIKA *PENDO LA KARAHA***

2. 1 Utangulizi ................................................................................................ 11

2. 2 Ukabwela Katika *Pendo La Karaha* ........................................................ 11

2. 3 Ubwanyenye Katika *Pendo La Karaha* ................................................... 15

2. 4 Matumizi ya madawa ya kulevya .............................................................. 20

2. 5 Dhiki za ajira ng`ambo ............................................................................. 22

2. 6 Kutowajibika kwa Serikali ......................................................................... 25

2 . 7 Hitimisho .................................................................................................. 29

## SURA YA TATU

## NAFASI YA VIJANA KATIKA *PENDO LA KARAHA*

3. 1 Utangulizi....................................................................................................31

3. 2 Nafasi chanya wanazopewa vijana ......................................................................31

3. 2. 1 Vijana na Uhuru wa mawazo..................................................................32

3. 2. 2 Vijana na maadili.....................................................................................33

3. 2. 3 Vijana na ari ya kujikomboa kiuchumi ....................................................34

3. 2. 4 Vijana na majukumu ya kuwatunza wazazi .............................................35

3. 2. 5 Vijana kama mihimili ya taifa..................................................................36

3. 3 Nafasi hasi wanazopewa Vijana ...........................................................................38

3. 3. 1 Uhusiano wa vijana na wazazi wao .........................................................38

3. 3. 2 Vijana na ukosefu wa maadili..................................................................39

3. 3. 3 Vijana na kisasi kazini ..............................................................................40

3. 3. 4 Vijana na dhuluma ...................................................................................41

3. 3. 4. 1 Dhuluma za kikazi ..................................................................41

3. 3. 4. 2 Dhuluma za mapenzi ...............................................................42

3. 3. 5 Ushindani na Ushawishi wa vijana..........................................................43

3. 4 Hitimisho...............................................................................................................44

## SURA YA NNE

## TATHMINI YA HALI YA JAMII KATIKA *KOVU MOYONI*

4. 1 Umaskini katika riwaya ya Kovu *Moyoni* ..........................................................46

4. 2 Ubwanyenye katika *Kovu Moyoni* .........................................................................46

4. 3 Vijana na madawa ya kulevya ...............................................................................47

4. 4 Dhuluma na unafiki wa viongozi walio mamlakani ..............................................48

4. 6 Maovu ya ubakaji na unajisi ..................................................................................53

4. 7 Athari ya ukosefu wa ajira .....................................................................................53

4. 8 Hitimisho................................................................................................................54

## SURA YA TANO

## NAFASI YA VIJANA KATIKA *KOVU* MOYONI

5. 1 Utangulizi........................................................................................................55

5. 2 Vijana na ari ya Kujikomboa Kiuchumi ..........................................................55

5. 3 Vijana na uzalendo...........................................................................................56

5. 4 Nafasi hasi wanazopewa Vijana ......................................................................58

5. 4. 1 Vijana na Maovu..........................................................................................58

5. 5 Hitimisho..........................................................................................................61

## SURA YA SITA

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

6 . 1 Utangulizi......................................................................................................62

6. 2 Muhtasari wa matokeo ya utafiti.......................................................................62

6.3 Changamoto za utafiti .......................................................................................66

6.4 Hitimisho...........................................................................................................66

6. 5 Mapendekezo ....................................................................................................66

**MAREJELEO** .........................................................................................................67

## KUTABARUKU

Namtabarukia marehemu mamangu mzazi Ann Nyambura.

Malezi yako na nidhamu uliyodhamini kwetu imekuwa ni dira yangu muda huu wote. Ulijinyima mengi katika maisha yako kwa sababu ya masomo yangu. Nani kama wewe mama ?. Mola ailaze roho yako pema peponi.

## SHUKRANI

Ukamilifu wa tasnifu hii haungekamilika pasipo na mchango wa watu mbalimbali. Kwa Mola mwumba wangu, ni mkono wa tahania kwa kuniongoza kutoka mwanzo hadi sasa.

Shukrani za dhati na maalum ni kwa wasimamizi wangu Prof. Mwenda Mbatiah na Dkt. Evans Murage Mbuthia. Hawa wamekuwa wasimamizi wa kupigiwa mfano. Ushauri wao umeufanikisha utafiti huu. Mola awe nanyi siku zote za maisha yenu.

Shukrani zingine nazitoa kwa wahadhiri wangu wengine katika idara ya Kiswahili katika Chuo kikuu cha Nairobi ambao walinisaidia na kunielekeza katika kazi hii ya usomi. Hawa ni: Prof. John Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Amiri Swaleh, na Dkt. Jerono. Sitamsahau kwa njia ya kipekee Prof. Aswani Buliba wa Chuo Kikuu cha Laikipia. Mwongozo na ushauri wako ulinifaa pakubwa. Mola awe dira siku zote za maisha yenu.

Kama si wewe mke wangu Martha, chombo changu kingeenda mrama. Ulinihimiza na ukanivumilia nilipokuacha peke yako na kuzama kwenye mabuku. Wewe umekuwa `kito` katika maisha yangu. Wanangu Faith, Chris na Ann mlivumilia kwa kutokuwa nanyi mliponihitaji. Langu sasa ni kuwaombea baraka na neema zake Mola ziwe nanyi siku zote.

Sitowasahau wanafunzi wenzangu: Kimetto, Kelvin, JohnBosco, Asha, Emmily, Nduku Caroline, Kimeu, Jacklyn, Mangistu, Meshack, Silveria, Chesebe, Zahra, Wangeci, Faith, Waweru, Chepkorir, Bi. Gitonga, Xariun, Lydia, Mogusu, Bosibori, Jared, Kemunto, Winnie, Lilian Anyango na Polycap Adika. Nawashukuru kwa dhati ya moyo wangu, Mungu awajalie neema yake mnapopanda ngazi hii ya masomo.

Namshehenezea shukrani mwalimu mkuu wa shule ya Jacaranda Bi. Kariuki Beatrice. Ulinielewa na kunisaidia kila nilipotaka kwenda katika shughuli za masomo haya. Neema ya Mola iwe nawe siku zote. Kwa walimu wenzangu: Karanja na Danson kwa kuniongoza katika upigaji chapa, Kimani, Kibathi, Mwangi, Kamau, Tr. Vero, Kibe, Bi. Josphine, Ole Nampaso, Bonface, Robbert, Mbugua, Eunice, Rufus, Naomi, Zippie, Rachael, Githinji na Kimathi. Nyote mumekuwa watu wa maana sana kwangu. Nayo neema yake Mola iwe nanyi daima.

Shukrani za dhati ni kwenu EDKAM maili kumi-Bahati mliyeipiga chapa kazi yangu ya mwanzo. Mlinielekeza vyema jinsi ya kuendelea kuboresha upigaji chapa wa sura zilizofuatia. Kwenu nasema Mola awe dira ya kazi yenu na awazidishie neema na hekima katika shughuli zote mzifanyazo.

Nawashukuru wote waliohusika kwa hali yoyote ile, mlikuwa msaada kwangu. Japo sikuwataja kwa majina, nasema asanteni sana na Mungu awabariki.

## IKISIRI

Tumeangazia nafasi ya vijana katika riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni* za John Habwe. Hata hivyo ilitubidi kusoma riwaya nyinginezo za mwandishi huyu kama vile *Hadaa ya Nafsi* na *Safari ya Lamu* ili tupate ufahamu zaidi kuhusu mwelekeo wa uandishi na falsafa ya msanii huyu. Tulichagua mada ya nafasi ya vijana katika riwaya zilizohusika, kwanza kwa sababu nafasi ya vijana inaonekana kudhihirisha na kuakisi hali ilivyo katika jamii zetu. Hii ni kwa sababu jamii zetu zina mchango mkubwa katika hali ya maisha ya vijana. Tulilenga vilevile kuchunguza changamoto zinazowakabili vijana katika jamii na kuwazuia katika juhudi zao za kujikomboa kutoka katika matatizo mengi kama ukosefu wa ajira na usambazaji wa dawa za kulevya. Aidha ubinafsi, dhuluma za mapenzi kutoka kwa waajiri, unafiki wa viongozi, utabaka uliokithiri na umaskini ni baadhi tu ya changamoto wanazokumbana nazo vijana kwenye jamii. Utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya Uhalisia Hakiki tukijikita katika kiunzi chake cha tatu kinachodai kuwa matukio au mambo yanayotendeka katika jamii hutendeka kwa kusababishwa na mambo fulani wala hayatokei tu vivi hivi. Kila tukio lina chanzo chake. Mwongozo huo umetufanya kuitathmini jamii mwanzo kabla ya kuitalii nafasi ya vijana katika riwaya zinazohusika. Kutokana na utafiti wetu, imebainika kuwa John Habwe amefaulu vilivyo katika kuwasawiri vijana na nafasi hasi na chanya wanazochukua katika jamii iliyojaa adha ya ubinafsi, uchochole, udhalimu, utabaka, na unafiki katika kutaja maovu machache. Aidha mwandishi ametoa mchango wake muhimu katika kuwajenga vijana kihadhi.

# SURA YA KWANZA

## 1. 1 Usuli wa Mada

Utafiti huu unahusu nafasi ya vijana katika riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni* za John Habwe. Kamusi ya Kiswahili Sanifu TUKI (2013) inaelezea kijana kama mtu wa makamo mwenye nguvu. Inaeleza zaidi kwamba huyu ni mtu aliye katika kipindi cha maisha kati ya utoto na utu uzima. Kulingana na jarida la *The World Youth Population (1995)* lililochapishwa na Umoja wa Mataifa, kijana ni mtu aliye kati ya miaka 15 na 24. Jarida hili lilikadiria kuwa idadi yao kwa wakati huo ilitimia bilioni moja nukta tatu sawa na asilimia kumi na nane ya idadi ya watu duniani.

Ufafanuzi wa maana ya dhana ya kijana unatofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Kulingana na Becker (2011) ujana ni kipindi cha mpito toka hali ya utoto hadi utu uzima. Anasema kuwa hiki huwa ni kipindi ambapo mabadiliko mbalimbali hutokea ndipo mtoto awe mtu mzima. Ni wakati mahususi ambao mabadiliko haya hutokea ingawa si bayana kwa mtu binafsi kwani jamii tofautitofauti huwa na mitazamo mbalimbali ya kitamaduni kuhusu mabadiliko hayo kwa namna zinavyotambua na kuwapa vijana mamlaka na uwezo wa kimaamuzi. Fasili zenye misingi ya kitamaduni, mila na desturi huzua utata na mkanganyiko mkubwa sana katika kuielewa dhana nzima ya vijana kulingana na Becker.

Nafasi huelezwa kama mahali palipo patupu na ambapo panaweza kuwekwa kitu. Ufafanuzi huu ukiwekwa katika muktadha wa kijamii una maana kwamba kila mmoja ana mahali pake alipotengewa na jamii ili apate kushiriki katika mambo ya kijamii. Mwandishi amelishughulikia kundi hili la vijana kwa kiasi kikubwa na hasa changamoto zinazowakabili hapa nchini Kenya pamoja na mataifa mengi barani Afrika na katika mazingira wanamojikuta ya ukosefu wa ajira.

Ulevi, matumizi ya dawa za kulevya na tamaa kubwa ya kutaka kukimbilia mataifa ya Ughaibuni hususan Saudi Arabia pamoja na kutumiwa vibaya na viongozi wa kisiasa, ni baadhi tu ya matatizo wanamojikuta vijana ambao ni kundi muhimu sana katika jamii. Umuhimu huu unatokana na sababu kadha. Kwanza, wao ndio wanaounganisha kizazi cha sasa na kile kinachokuja. Hivyo basi kutolishughulikia kundi hili ni sawa

na kutoijali kesho ya watoto wetu. Pili vijana wanawakilisha asilimia kubwa sana ya idadi ya watu nchini Kenya. Kulingana na *Youth Challenge International (2009)* asilimia sitini ya watu nchini Kenya haina ajira. Huku ni kumaanisha kuwa idadi kubwa ya watu kwa jumla inajengwa na vijana. King'ei na Kobia (2007:325) katika jarida la *Nordic Journal of African Studies* wameshikilia msimamo huo huo kuwa zaidi ya asilimia sitini ya idadi ya watu nchini Kenya ni vijana, hivyo basi kuwaelewa pamoja na changamoto zinazowakumba kutamaanisha kuyaafikia maazimio mengi ya jamii na kuafikia utangamano katika masuala mengi yanayoihusu jamii.

Mbali na idadi yao kubwa, vijana wanawakilisha uhai wa taifa. Katika uhai tunamaanisha kwamba hali ya siku zijazo ya taifa inawategemea wao kama msingi wa kizazi cha baadaye. Katika maisha ya jamii siku za nyuma, maadili yalisambazwa na kuhimizwa miongoni mwa vijana. Kwa mfano, vijana hawakuruhusiwa kuhusiana kimapenzi na watu waliowazidi umri. Haya na mengine mengi yanadhihirika miongoni mwa vijana kama ilivyochorwa katika riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni*.

**1. 2 Tatizo la Utafiti**

Mengi ya matatizo na changamoto zinazowakumba vijana zinatokana na jamii wanamokulia. Hii ni kwa kuwa vijana wanakulia katika jamii iliyojaa maovu kama vile unafiki, ufisadi, ubinafsi na tofauti za kitabaka. Pengo tunalonuia kuziba katika utafiti huu ni kuchunguza aina za nafasi za vijana katika jamii ya aina hii. Utafiti huu basi ni jaribio la kuchunguza harakati ya vijana katika juhudi zao za kujaribu kujikomboa kutokana na matatizo na dhiki mbalimbali zinazowakumba wakijaribu kujiendeleza.

Bila ya kuwatenga katika misingi ya kijinsia, tunawaangazia vijana wote wanaosakamwa na changamoto za ukosefu wa ajira na wengine wao kuingia katika kinamasi cha dawa za kulevya. Hayo yanapowatendekea ni muhimu tuangazie nafasi zao katika riwaya zinazohusika.

### 1. 3 Malengo ya Utafiti

i. Kufafanua nafasi ya vijana katika riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni*.
ii. Kuchunguza changamoto zinazowakabili vijana katika riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni*
iii. Kubainisha kufanikiwa au kutofanikiwa kwa uwasilishaji wa maudhui ya nafasi ya vijana katika riwaya zinazohusika.

### 1. 4 Maswali ya Utafiti

i. Vijana wana nafasi gani katika jamii kulingana na riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni ?*
ii. Ni changamoto zipi zinazowakabili vijana katika jamii kulingana na riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni ?*
iii. Je, uwasilishaji wa maudhui ya nafasi ya vijana katika riwaya zinazohusika umefaulu kwa kiasi gani?

### 1. 5 Sababu za kuchagua mada

Tumechagua mada hii kwa sababu kadha. Kwanza riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni* zimechapishwa mwaka wa 2014. Hivyo tukapata msukumo wa kutaka kuzitalii kazi hizi mpya ambazo hazijashughulikiwa kitaalamu.

Tumeichagua mada hii vilevile kwa sababu nafasi ya vijana inaonekana kudhihirisha na kuakisi hali ilivyo katika jamii zetu. Hii ni kwa sababu jamii ina mchango mkubwa katika hali ya maisha ya vijana kwa kuwa wanakulia miongoni mwao na kuwa na tajriba kubwa ya maisha yao.

Tumechagua mada hii ya nafasi ya vijana kwa sababu Katiba mpya ya Kenya (2010) inaangazia mojawapo ya changamoto zinazoikumba jamii ya vijana ambayo ni ufisadi. Ufisadi katika jamii unachangia katika nafasi za vijana nao unaangaziwa kwenye katiba hii katika sura ya sita sehemu ya sabini na tatu, ibara ya pili kipengele cha (b).

Tumechagua mada hii vilevile kwa sababu ulimwengu wanamojikuta vijana, wawe ni wa kike au kiume, ni ulimwengu wao kwa pamoja na changamoto zao kama vijana ni zile zile.

### 1. 6 Upeo na mipaka ya Utafiti

Utafiti wetu unajikita katika riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni* ambapo tunaangazia *nafasi ya vijana.* Mbali na riwaya hizi, tumesoma pia riwaya nyingine za mwandishi huyu kama vile *Safari Ya Lamu* (2011) na *Hadaa ya Nafsi* (2014) ili tuupate mwelekeo wa uandishi wake. Hatukuongozwa na kigezo chochote kile katika kuziteua riwaya hizo mbili ila ni kwa sababu zinagusia maswala mengi yanayowahusu vijana sawa na riwaya nyinginezo za mwandishi huyu. Kufanya hivi kunatusaidia kutathmini nafasi ya vijana katika kazi zake kwa jumla. Imebidi tutaje vitabu vingine vilivyoandikwa na waandishi wengine kwa ajili ya kutoa mifano inayohusiana na kazi yetu.

### 1. 7 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu umefanywa katika misingi ya nadharia ya Uhalisia Hakiki.
Mbatiah (2001) anasema *Uhalisia Hakiki* ni aina ya uhalisia ambapo fasihi inayohusika imelengwa kuihakiki jamii. Anaendelea kusema kuwa Uhalisia Hakiki hushambulia mfumo wa kibepari ambao ni chanzo cha uozo wa jamii. Makabwela huwa wanatetewa kwani wanakandamizwa na mfumo huo wa kibepari.

Nadharia ya Uhalisia Hakiki basi husisitiza umuhimu wa kuyaelewa mambo kwa kuyahakiki. Uhalisia hakiki ulipendekeza viunzi vitatu vya uhalisia, Collier, (1994:42-45). Cha kwanza kinahusu yale tuliyozoea katika maisha yetu ya kila siku. Yale tunayoyaona na kupata tajiriba kuyahusu katika ulimwengu.

Kiunzi kingine ni kile kinachohusu matendo na matukio mbalimbali**.** Ni yale mambo yanayotendeka katika ulimwengu huu tunaouona na kuutambua. Ni yale yanayotendeka na kusemwa.

Kiunzi cha tatu ndicho muhimu zaidi katika mada tunayoshughulikia. Kiunzi hiki kinahusu taratibu za kufanya mambo. Kinadai kwamba matukio au mambo

yanayotendeka katika jamii hayatendeki tu vivihivi bila kusababishwa na chochote, lazima matukio yawe yameanzishwa au kusababishwa na jambo fulani.

Tathmini ya wanauhalisia Pawson na Tilley (2002) ilishikilia pia msimamo huohuo juu ya nadharia hii. Walizungumzia kuhusu matukio muhimu. Wanasema huenda pakawa na matukio mbalimbali ambayo yanawezekana yakawa sio wazi na yamejificha yasionekane waziwazi na mtazamaji. Matukio hayo mbalimbali huchochewa na hali iliyopo katika jamii ambamo mambo yanatokea na hali ya mambo yenyewe na wala sio sababu zingine. Tathmini hii ya Pawson na Tilley inadai kuwa taratibu za kufanya mambo yanayochochewa na mazingira yanakotokea huleta matokeo yanayoweza kuwa ni ya kupendeza (chanya) na yasiyopendeza (hasi).

Msingi mkuu wa tapo hili ni usimulizi wa matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inayokaribiana sana na hali iliyoko katika jamii (Wamitila 2002:115). Mwandishi kwa hivyo anapaswa kuyaakisi maisha ya jamii katika ngazi ya kijamii, kiuchumi, kitamaduni na kisiasa. Uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Waandishi wanaoandika katika msingi huu wanatarajiwa kwa hivyo, kutoa picha za wahusika, matukio na mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisi wa jamii ya mwandishi anayehusika. Mwandishi anatilia mkazo wahusika katika hali za kawaida za maisha, matukio na mandhari ya kawaida au yanayoweza kuonekana katika jamii. Huu ndio msingi hasa wa kauli ya Lenin kuwa fasihi ni kioo cha jamii, kama anavyonukuliwa na Wamitila (2002).  Haja kubwa ya kuigiza ilikuwa kuonyesha picha ya mazingira ambamo jamii inapatikana mathalan, kioo kitumikavyo kuonyesha picha za mwanadamu. Hivyo basi mwandishi aitoe picha ya jamii bila kuidunisha wala kuipigia chuku.

Nafasi ya vijana tunayoangazia katika riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni* inachochewa na hali ya mazingira ambayo vijana wanajikuta ndani yake. Ukweli ni kwamba ijapokuwa fasihi huzungumzia ukweli, mwandishi huchagua mambo anayotaka kuzungumzia. Mwandishi huchagua, akachanganua na kutenganisha anayozungumzia. Mwandishi wakihalisia huweza kusuta maovu ya kijamii.  Baadhi ya waandishi huonyesha misimamo yao juu ya lile wanalozungumzia. Hapa ndipo tunapouona uhalisia ambapo pamoja na msanii kujizatiti kuchora hali halisi ya maisha

kama yalivyo, hutetea tabaka au kundi fulani na kulishambulia lingine kutegemea msimamo wake. Katika kufanya hivyo, si lazima mwandishi awe na itikadi maalumu na bayana kuhusu maisha. (Wamitila 2002)

Kanuni kuu za Uhalisia Hakiki zinaweza kutajwa kwa ufupi kama ifuatavyo:
Pawe na uelewa na ufahamu kwamba matukio yatendekayo katika jamii huwa na visababishi vyake na kwamba mambo au matukio kama hayo hayawezi kutokea tu. Lazima pawe na chanzo.

Uhakiki wa matukio mbalimbali katika jamii uwe ni wa kufanyika kulingana na uzoefu au tajriba ya binadamu katika mazingira yake.

Usawiri wa matukio kihistoria pale ambapo wahusika wanatekeleza matendo yao kitabaka aidha kimakusudi au bila kufahamu.

Kuyafahamu na kuyaelewa matukio na masuala mbalimbali katika jamii iwe ni baada ya kutathmini hali ya maisha ya jamii hiyo.

### 1. 8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Mogambi (1983) alihakiki kilio cha wanyonge hususan vijana kama inavyojitokeza katika riwaya tatu za S. Mohamed za *Asali Chungu* (1978), *Dunia Mti Mkavu* (1980) na *Utengano* (1980). Anapotuonyesha jinsi wanyonge wanavyodhalilishwa na jamii, anatupa uelwa mzuri wa changamoto ziwakumbazo vijana kwa jumla. Uhusiano mwingine wa kazi hii na yetu ni kwamba tumewachukulia vijana kama kundi ambalo linadhalilishwa na jamii katika *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni* . Anapodhihirisha mambo yale ambayo yanachangia unyonge wao, anatusaidia kutafiti masuluhisho ambayo yanahitajika ili kukabiliana na kuondoa unyonge huu.

Lugano (1989) aliangalia namna Kezilahabi alivyowachora wahusika wa kike na ikikumbukwa kwamba Kezilahabi aliangazia zaidi wahusika vijana kama vile Kazimoto katika *Kichwa Maji* (1974) na *Rosa* katika *Rosa Mistika* (1971). Kazi hii imetupatia msaada mkubwa. Hata hivyo, badala ya kuwashughulikia tu wahusika wa kike, sisi katika utafiti wetu tunaangazia vijana kwa jumla. Katika kufanya hivyo

tunawasilisha picha inayoonyesha hali halisi ambayo inahusiana na matatizo yanayowakumba vijana, wawe wa kike au wa kiume.

Kruger (1998) alitafiti kuhusu usawiri wa wanawake kulingana na waandishi wa Kiafrika walioandika riwaya na hadithi fupi. Alisema kwamba waandishi hawa hawatumii wahusika wanawake kama wahusika wakuu bali huwatumia kama wahusika wajenzi. Kinyume na alivyosema Kruger, utafiti wetu unahusisha vijana kwa jumla. Vile vile nafasi ya vijana tunayoiangazia inachukuliwa zaidi na wahusika wote kama wahusika wakuu.

Katola (2006) alitafiti kuhusu udhalimu wa wahusika wanawake katika tamthilia za Kiswahili. Alishughulikia tamthilia za Ali Katini Mwachofi, *Mama ee* (1987), Penina Muhando, *Hatia* (1972), A.S Yahya na David Mulwa, *Buriani* (1983) na Said Ahmed Mohamed, *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000). Alishughulikia swala la udhalimu wa wanawake kwa jumla huku akirejelea katika waandishi wa kiume na wale wa kike. Utafiti wetu umejikita katika riwaya na kuangazia nafasi ya vijana wote, wawe ni wa kike au kiume bila kuwabagua. Hivyo basi, utafiti wa Katola umetufaa kwa kutupa mwangaza kuhusu yale tunayotafitia.

Mutua (2007) aliangazia mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke katika tamthilia tatu za Kiswahili. Kilichotuelekeza kupitia kazi hiyo ni mitazamo ya vijana katika ukombozi wa wanawake. Hata hivyo, tulionelea kwamba mkabala huo wake ulikuwa umejikita katika ukombozi wa wanawake pekee. Katika utafiti wetu, tulihisi kwamba ukombozi ambao vijana wanahitaji uwe ni wa malezi, ajira, elimu, maadili na umaskini unafaa kushughulikia vijana wote bila kujali jinsia zao.

Masibo, B. (2009) katika *Gendered Perspectives in the Novels of Ngugi wa Thiong'o and Alice Walker*, analinganisha fasihi iliyoandikwa na Mwafrika wa kiume Ngugi wa Thiong'o na Mmarekani mweusi wa kike kuhusu taswira ya mwanamke na mwanamume. Masibo anachanganua na kulinganisha taswira chanya na hasi zilizopewa mwanamke. Kazi hii imetufaa katika utafiti wetu kwani sisi tunaangazia nafasi ya vijana, wa kike na wa kiume kwa jumla.

Mirikau (2011) katika tasnifu yake ya uzamili aliangazia swala la taswira ya mwanamke katika tamthilia tatu za Kiswahili: *Wingu la Kupita* (1999), *Pango* (2003) na *Seserumbe* (2009) za K.W. Wamitila. Alizungumzia usawiri chanya na hasi wa mwanamke. Usawiri huu wa mwanamke umetuwezesha sisi kuangazia changamoto na dhuluma zinazowakabili vijana wote, wa kike na wa kiume kwa pamoja na nafasi zao katika jamii na mikakati yao katika kujikomboa kutokana na dhuluma wanazokumbana nazo. Mirikau alitumia tamthilia tatu lakini sisi tumejikita katika riwaya mbili za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni*.

Kiongera (2012) alishughulikia mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya katika tamthilia za Kiswahili kama vile *Kifo Kisimani* (2001), *Pango* (2003), *Maua kwenye Jua la Asubuhi* (2004) na *Seserumbe* (2009). Ingawa mhakiki huyu alitumia tamthilia kuonyesha mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya, haya yanatufaa sana kwani matukio kama si chanya ni hasi.

Naliaka (2012) katika kazi yake alishughulikia uhakiki wa hali ya vijana katika *Vipanya vya Maabara*. Katika utangulizi wake alieleza waziwazi matatizo yanayowakumba vijana katika jamii na chanzo chake. Alitoa mfano wa Muli na sababu ya kubobea madawa ya kulevya ambayo ni kukosa baba mzazi wa kumwelekeza. Ni sababu kama hizi zinazowafanya vijana kujikuta katika hali mbalimbali katika riwaya tunazozitafitia, hasi na chanya.

Manoti (2012) alishughulikia dhamira ya uozo na athari zake kwa jamii katika *Upotevu* (2005). Manoti anafafanua kwa undani dhamira ya uozo katika riwaya ya Upotevu na kuonyesha wazi jinsi mwandishi wa riwaya hii alivyosawiri jamii husika. Aidha alionyesha jinsi mtunzi wa riwaya hii alivyoubainisha uozo katika jamii yake kwa uwazi na ukamilifu. Matokeo ya utafiti wa Manoti ni ya manufaa sana kwetu kwa sababu mbali na kuangazia nafasi ya vijana katika riwaya tunazoshughulikia, tunaitathmini jamii vilevile.

Obore E.M. (2012) alitafiti kuhusu dhuluma dhidi ya vijana wa kike katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) na *Tumaini* (2006). Alisema kwamba swala la dhuluma dhidi ya vijana wa kike linabainika wazi katika riwaya hizo na swala hilo limejitokeza kwa

hali mbalimbali na kudhihirisha kuwa vijana wa kike wamekandamizwa na kunyimwa haki. Hali hii imebainika kutokana na sababu ya kuonekana kwa kijana wa kike kama kiumbe duni na jinsia ya kiume yenye misingi na kaida zenye mashiko katika mila na tamaduni zinazompendelea kijana wa kiume. Kazi hii ya Obore imetufaidi mno katika utafiti wetu kwa sababu imeshughulikia maswala ya vijana wa kike hasa jinsi kijana huyu wa kike amedhulumiwa na kukandamizwa bila kupewa haki inayostahili kama mtoto wa kike. Tofauti na kazi yetu ni kwamba yeye aliangazia dhuluma ya kijana wa kike wakati sisi tukiangazia changamoto za vijana wote, wa kike na kiume. Pili, alijihusisha na riwaya mbili za wandishi tofauti sisi tukijikita katika riwaya mbili za mwandishi mmoja.

**1. 9 Mbinu za Utafiti**

Kimsingi utafiti wetu umekuwa ni uhakiki ambao umefanyiwa maktabani. Hivi ni kwa sababu utahusu kusoma na kuzihahiki riwaya nyinginezo za John Habwe kama vile *Safari ya Lamu* (2011) na *Hadaa ya Nafsi* (2014) kando na riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni*. Japo hizo sio riwaya pekee za mwandishi huyu, tumezisoma tu kwa kutaka kuongeza ufahamu zaidi juu ya kazi zake kwa jumla pamoja na kuwa kuzisoma kazi zake kumetupa ufahamu juu ya falsafa ya mwandishi huyu.

Tumerejelea vitabu, makala na maandishi yanayohusu nadharia ya Uhalisia Hakiki tunayotumia katika utafiti wetu. Tumerejelea tasnifu za viwango vyote zilizoandikwa kuhusu Uhalisia Hakiki katika kazi za kifasishi. Pia tumetumia tovuti kwenye mitandao tofauti inayokubalika ya kiusomi ili kupata yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya Uhalisia Hakiki. Tumetekeleza haya kwa lengo la kupata uelewa wa kutosha kuihusu nadharia hii ya Uhalisia Hakiki.

Sampuli tuliyoteua ni sampuli lengwa ambayo ni riwaya za Habwe. Kulingana na Mugenda na Mugenda (1999:50) aina hii ya sampuli humwezesha mtafiti kutumia kadhia ambazo zina ujumbe kulingana na maudhui ya utafiti. Sampuli lengwa huchaguliwa kwa sababu fulani maalum. Mtafiti hukusudia kupata habari za kina kuhusu suala fulani.

Data tuliyoipata tuliichanganua kulingana na malengo yetu na mihimili ya nadharia ya Uhalisia Hakiki. Baada ya kuikusanya data yetu, tumewasilisha matokeo ya utafiti wetu kwa njia ya maelezo.

Imetulazimu vile vile kuwahusisha wataalamu mbalimbali na wasanii ili watupe mwanga zaidi kuhusu maswala mbalimbali ambayo yametufaidi katika utafiti huu.

# SURA YA PILI

## TATHMINI YA HALI YA JAMII KATIKA *PENDO LA KARAHA*

### 2. 1 Utangulizi

Sura hii inahusu kutathmini hali ya maisha na maswala ya kijamii katika *Pendo la Karaha*. Hili linatendeka kwa kuongozwa na kuelekezwa na nadharia yetu ya Uhalisia Hakiki na hasa kiunzi chake cha tatu. Hiki kinadai kuwa matukio katika jamii hutendeka kwa kusababishwa na masuala mbalimbali (Bhasker 1998). Maisha na hali ya jamii ndio inayosababisha vijana kujipata katika hali walizonazo. Matukio tunayorejelea na kutarajia ni hizo nafasi zinazochukuliwa na vijana, aidha ni chanya au hasi. Kwa hiyo, maisha na hali ya jamii ndiyo huelekeza na kusababisha nafasi mbalimbali za vijana.

### 2. 2 Ukabwela Katika *Pendo La Karaha*

Ukabwela ni umaskini au uchochole. Hali hii inadhihirika kupitia kwa wahusika wakuu na wahusika wadogo. Kudra ni mhusika mkuu mmojawapo. Maneno na matendo yake yanadhihirisha hali duni ya maisha ya jamii ya makabwela katika riwaya hii. Mwandishi anaelezea kuwa familia yake ilikuwa imechapwa viraka vya umaskini hohehahe (uk 1). Anaendelea kutuangazia hali ilivyo katika familia ya mhusika mkuu Kudra. Anaeleza kuwa baada ya kifo cha babake Kudra, Bw. Sanga aliyefanya kazi bandarini, mamake Kudra aliingilia biashara ya kuuza mbaazi, maharagwe, vitumbua na sambusa. Mwandishi anasema:

> Biashara hii haikua na faida kubwa.
> Hata hivyo, Riziki na Mwanawe walikula,
> wakalipa kodi ya mwenye nyumba
> na kufanya shughuli nyingine
> ndogondogo ( uk 3).

Kazi aliyofanya mamake Kudra ilikuwa ni ya bora mkono wende kinywani. Mawazo mengi juu ya umaskini wao yaliwajia akilini mwao kila uchao. Walijiuliza maswali mengi katika juhudi za kutafuta chanzo cha shida zao. Kudra anajisemesha yeye na nafsi yake akijiuliza ni lini angetoka katika maisha hayo. Alishindwa kufahamu kama kila kinachowapata katika maisha yake ni kudura ya Mungu. Anashindwa kuamini

kama ni Mungu yupi huyo ambaye angekubali maisha yake yawe ni hayo ya kuhangaika (uk 3). Tunaonyeshwa hali ilivyokuwa pale katika sebule ya akina Kudra:

> Mara kwa mara, Kudra alikaa katika
> Kochi bovu lililoraruka na kuonyesha
> wazi katani lake la mkonge la hapo kwao
> bandani akitafakari maisha yake (uk 4).

Baada ya Rukia kumpoteza babake Bw. Kipanga, aliyekuwa mvuvi maarufu kule baharini, maisha yaliwabadilikia. Subira mkewe na mwanawe waliyazoea maisha bila mkimu. Hata hivyo hali iliwawia ngumu jambo lililomfanya Rukia kuacha shule ili amsaidie mamake. Rukia sasa akawa anafanya kazi ya kuuza leso kwa Rajiv hapo Mombasa (uk 5).

Hali ya umaskini uliokuweko katika jamii uliwafanya vijana kuacha masomo ili kuwasaidia wazazi wao katika kutafuta riziki yao. Hali ya umaskini inamfanya Kudra kukata tamaa katika kutafuta elimu. Hana matumaini yoyote kwamba hata elimu hiyo ingewatoa katika hali yao duni kwa sababu hata baadhi ya waliosoma hawakuwa na kazi. Kudra alimueleza mamake kuwa yeye mwenyewe hakuona dau la elimu likiwa na maslahi. Aliona kama ni dau la mnyonge. Akashindwa kwa nini hata waliosoma walikosa kazi (uk 6).

Mtunzi wa riwaya ya *Pendo la Karaha* anamtumia mamake Kudra Bi. Riziki na kutuchorea picha ya baadhi ya kazi duni walizofanya ili kujipatia riziki yao. Kwamba alipambana na moto uliomwachia mabaka ya alama mkononi. Jioni ilipofika akawa anauza mchicha na kunde kwa wapita njia hapo Likoni (uk 1).

Maelezo haya ya mwandishi yamekusudiwa kutuonyesha jinsi jamii hii ilivyopambana na hali duni ya maisha. Wanajamii walifanya kila juhudi ili kujikimu maisha yake kwa hali na mali. Ilifanya kila ililoweza ili kuendeleza maisha yake. Hali ilikua si hali katika maeneo ilimoishi jamii hii. Wazazi walilalamikia mazingira mabovu na vilevile vijana wao walioingilia madawa ya kulevya. Riziki alipomtembelea Subira huko alikohamia katika mtaa wa juu ulioitwa Amsterdam na kuulizwa hali yao katika mtaa wa mabanda wa Likoni, Riziki alimjibu kuwa matatizo ya kukosa maji yalikuwa ni yale yale pamoja na umeme uleule wa kupimiwa na vyoo vichafu. Hii akasema ndiyo iliyokuwa ni hali yao ya kulalamika kila siku.

Akaongezea pia kuwa hata na jinamizi la dawa za kokuteli, unga na bangi halikuwaondoka (uk 15).

Maeneo ya Likoni alimoishi Riziki na mwanawe Kudra yalikuwa ni maeneo ya mabanda na ya ovyo. Maeneo yao yalivuja wakati wa mvua nyingi. Riziki na Kudra hawangeweza kuhamia katika maeneo bora kwa kuwa hawakuwa na uwezo wa kiuchumi. Tunaelezwa kilikuwa ni kipindi cha mvua nyingi Mombasa, mvua zilizobomoa nyumba. Riziki alipatwa na wasiwasi wa nyumba yake iliyovuja ajabu. Nyumba haikuwa yake na hangeweza kuhamia kwingine kwa sababu ya kodi za juu za nyumba hizo mjini Mombasa. Alisema kuwa tayari nyumba yake ya Likoni alidaiwa kodi ya miezi sita. ( uk 101 ).

Mwandishi anawatumia vijana wawili wa kike, Lindo na Kudra kuendelea kutudhihirishia hali ya ukabwela ulioigubika jamii yao. Baada ya Kudra kupokea habari za kifo cha rafiki yake Lindo, Kudra alilia sebuleni alikokalia ndoo ya maji iliyozeeka. Kudra alimkumbuka rafiki yake Lindo hasa alipoingia katika mojawapo ya mabanda ya pale kwao. Aliingia nyumba moja iliyoinama upande mmoja. Nyumba hii ingeanguka wakati wowote. Mabati yake yalionekana kwa nje na makuti nayo yaliyoezeka paa lake yalioza ( uk 32-33 ).

Maneno anayosema Lindo akijisemesha mwenyewe baada ya kulewa dawa iliyotiwa kwenye chupa ya soda, yanaonyesha kwamba jamii yake iligawika kitabaka. Palikuwa na mawaziri matajiri na watoto wao walifurahia maisha ya starehe. Lindo aliisemesha soda hiyo na kuiambia isimuumize kwa kuwa yeye ni mtoto wa wenyewe hata kama baba yake si waziri.

Hali ya utabaka kuwepo inadhihirika wakati mhusika Mwadime anapozungumza na nafsi yake kuhusu hali yake. Kwanza alishindwa kwa nini aliishi. Hakuona raha maishani. Akasema walio na raha ni watu wengine.

Tunaelezwa kuwa Kudra alipogombana na binti ya mwajiri wake aliyeitwa Hanawi, hatimaye huyo Salim mwajiri wake alimwandikia Kudra barua ya kumsimamisha kazi. Jambo hilo la kufutwa kazi lilionekana kumshtua Kudra. Hii ni kwa sababu alihitaji kazi kwa vyovyote ili aweze kumsaidia mamake aliyemwacha jijini Mombasa katika umaskini wake. Kudra hakuliamini jambo hilo hata kidogo hasa

anapokumbuka maisha ya uchochole waliyoyaishi nyumbani. Alijaribu kumsihi Salim abadilishe uamuzi wake, lakini wapi! Aliisoma barua mara nne mfululizo. Ubongo wake ulisimama, asijue jambo la kufanya (uk145- 146).

Kupitia kwa mhusika kwa jina Mwadime, maisha ya uchochole na hali duni ya maisha inaendelea kujitokeza. Tunaelezwa kuwa alifiwa na mkewe Bi. Mwajuma na kuachiwa watoto wawili kuwasumbukia. Alikuwa ni jirani yake Riziki waliyekaa naye hapo kwa wingi wa uchochole. Alioa wanawake kadha lakini hakuna aliyeishi naye. Hii ni kwa sababu hakuwa na uwezo wa kuwakimu wote. Kazi yake ya uvuvi haingemwezesha kuwapa vitu walivyohitaji. Uvuvi ulimpa kula lakini si kufanya jambo la zaidi. Alikuwa mlalahoi. Alirauka majini asubuhi na akakaa hadi usiku lakini ujira wa uvuvi kwake ukawa mdogo.

Kwa jumla umaskini katika jamii hii ulikuwa mwingi. Vijana waliacha shule wakakaa nyumbani kutafakari la kufanya. Waliobahatika kupata ajira japo ya ujakazi, waliishikilia licha ya mateso mengi kutokana na kazi nyingi walizofanyishwa. Hata wengi walishindwa kuwajulia hali wazazi wao au kuwa na wao walipohitajika kwa kukosa ruhusa kazini kwao. Walipotishiwa kuachishwa kazi kama hizo ni jambo lililowashtua kwa kushindwa ni lipi lingine ambalo wangefanya.

Suala la kuwepo mitaa ya mabanda katika maeneo ya kuishi linadhihirisha hali ya uchochole na ukabwela kwa ujumla. Kundi la wanawake na wanaume likiongozwa na Subira, Kidawa, Riziki na wanawake wengine, liliondoka likianzia Mwembe Tayari hadi Likoni kwenda katika mtaa wa Baghdad likipitia katika mazingira ya kutisha na kutamausha. Walikuwa ni waandamanaji kwenda kukiteketeza kijiji cha Baghdad. Waliteremka kwa njia ya mchanga iliyojaa uchafu wa mikebe, karatasi, vijiti, maganda ya matunda, maembe na maji machafu yaliyoshuka mtaroni kwa hasira na uchafu wa kila aina . Kulikuwepo pia na nyumba za udongo na mabati mabovu na yaliyochoka yalitumiwa kujenga kuta. Milango ya nyumba hizo ilikuwa ni ya mabati vilevile. Walipita kwenye mitaro ya maji machafu yaliyonuka uvundo wa ajabu (uk 39). Waliendelea na Wakateremka katika bonde fulani ambako nyumba za kuishi zilikuwa ni sehemu ya nchi ambayo hawakuizoea wala kuielewa. Nyumba za Baghdad zilikuwa vibanda. Nyingi zilitosha kuishi watu wawili kwa sababu ya udogo wake lakini zilikaa familia kubwa. Nyumba zenyewe zilikuwa za mabati. (uk 41).

Maelezo haya yanaaonyesha aina ya mazingira ambayo jamii ya *Pendo la Karaha* iliishi na kukulia. Umaskini ulikithiri ajabu. Baadhi ya waandamanaji waliokuwa katika kundi hilo lililokwenda kukitia moto kijiji hicho cha Baghdad liliwaonea huruma na imani wakaaji wa eneo hili kama dhihirisho kuwa umakini mkubwa uliwakumba wakaaji wake. Waliwakataza kuvichoma moto vibanda vyao kwa kuwa walionekana ni wahitaji sana.

## 2. 3 Ubwanyenye Katika *Pendo La Karaha*

Mbali na mitaa ya ovyo na ya kikabwela katika jamii ya *Pendo la Karaha*, ilikuwepo pia mitaa ya kifahari walioishi mabwanyenye. Hili linadhihirika kwa maneno ya mhusika Mwamba baada ya yeye kuingiliwa na Kidawa kuwa ndiye aliyewauzia vijana dawa za kulevya. Mwamba anakana na kusema:

> "Mimi ningekuwa na uwezo huo, nisingekuwa
> hapa nashona mikeka basi. Ningekuwa ninakaa
> nyumba kama wao. Dadangu ningekuwa Nyali
> ama ningekuwa huko Bamburi, waona?"

Mabwanyenye walikuwepo na wengine waliwatumia vijana vibaya. Rehema alikuwa bwanyenye na wakala aliyewatafutia vijana ajira za Uarabuni. Hakufanya hivi bila malipo ila alilipwa vizuri na waajiri waliokuwa Uarabuni baada ya yeye kuwatumia vijana hasa wa kike kwenda kuwafanyia kazi. Alimshawishi Kudra kwa kumweleza akubali kazi hiyo ya Uarabuni kwani hiyo ndiyo iliyokuwa kazi wala sio hivyo vibarua vyake visivyomfaidi.

Vilevile maisha ya kibwanyenye ya Rehema yanadhihirika wazi kupitia maelezo yaliyomhusu bibi huyu yanayotolewa na mwandishi mwenyewe anapotupa picha ya sebule yake na vyombo alivyokuwa navyo mle ndani. Anasema kuwa kinywani bibi huyu alikuwa na jino la dhahabu na kuwa alikaa katika nyumba ambayo haikuwa ndogo wala kubwa lakini iliyotiwa starehe za kila aina. Sebuleni mlikuwa na makabati ya bei. Meza nazo zilitangaza uwezo aliokuwa nao mama huyo. Katika vidole vyake vya mkono wa kushoto vilikuwa na pete za dhahabu ( uk 23-24 ).

Jannete ni kijana wa kike aliyetumia madawa ya kulevya sawa na wenzake akina Lindo na Kassim. Tunaonyeshwa mawazo ya Jannete kumhusu Kassim ambaye alikuwa kijana mvulana wa bwanyenye Rehema. Kwa maelezo ya mwandishi, Jannete aliwaza juu ya Kassim ambaye mamake alikuwa na pesa chungu nzima lakini hakuzitaka. Alifuata lake na kudura yake. Akawaza juu ya huyu Kassim ambaye mamake alikuwa na kila kitu. Mbali na pesa katika benki, alikuwa vilevile na magari na nyumba. Ndiye ambaye aliwasafirisha vijana kwenda Dubai, Saudia na Lebanon.

Mawazo haya ya mhusika Jannete yanaonyesha kuwa mamake Kassim ambaye ni Rehema alikuwa ni tajiri mkubwa pale na bwanyenye wa kupigiwa mfano. Utajiri wa Bi. Rehema uliendelea kudhihirika hata zaidi katika mabishano yaliyozuka baina ya Kassim na Lindo kwa fundi Mwamba walipokuwa wakicheza bao. Lindo alimwambia Kassim aache kumwonea hata kama yeye hakuwa na uwezo (uk 45). Lindo alijua kuwa Kassim alitoka katika familia iliyokuwa tajiri na alishuku labda ndiyo sababu kuu ya mwenzake Kassim kumwonea. Ukwasi na utajiri mkubwa wa Bi. Rehema unaonekana kwa kujenga nyumba nyingi mtaa mzima kwa kuwapeleka vijana Ughaibuni. Alinunua mabasi yakapewa jina, "Maisha ni hiari yako" (uk 56). Aliweza hata kuwa na ofisi yake alikofanyia kazi yake ya kuwanadi wasichana katika mataifa ya Ughaibuni. Ilikuwa kwenye njia ya Haile Selassie katika jengo la Monitor. Ni katika jengo hilo ambapo wasichana wengi kutoka Kisumu, Nairobi, Nakuru, Mombasa na kwingine walifika ili kunadiwa (uk 76).

Rehema aliondoka siku moja ili kwenda kumtafuta mwanawe Kassim aliyepotelea Bombolulu kwa ajuza mmoja. Msimulizi anaeleza kuwa gari lake la aina ya Volvo lilisimama hapo kwa Zinduna. Watu walistaajabu kumwona Zinduna akiwa na mgeni wa gari (uk 78). Gari lake halikuwa gari tu bali gari la kifahari. Hata watu walistaajabu kilichomleta tajiri huyu kwa mwanamke mzee maskini aliyejulikana kwa ulevi na shughuli za kuuza dawa. Msimulizi anaendelea kusema kuwa hakujiendesha mwenyewe mpaka hapo Bombolulu. Anasema kuwa alikuja na dereva wake na walipomkosa Kassim, yeye na dereva wake, George, walirudi nyumbani wakiwa wamevunjika mioyo. Waliporudi mara ya pili Kassim alimwambia mamake kuwa harudi nyumbani na wakae na huo utajiri wao wa kunadi watu ugenini. Akaongezea pia kuwa yeye hakutamani hayo mavolvo yao (uk 80 ). Maneno na vitendo vya Rehema vingali vikidhihirisha ukwasi wake. Hata mwanawe licha ya kuwa aliyatumia

madawa na ulevi mwingine, hakupata kupotea fahamu na kuelewa barabara utajiri aliokuwa nao mamake Bi. Rehema.

Siku ambayo Kassim alikubali kurejea nyumbani, mamake alifanya kila juhudi ili kumsaidia kuuacha ulevi na matumizi ya dawa. Alimtia katika kituo cha kurekebisha tabia cha hapo Mombasa. Hata hivyo, mara nyingi Kassim alitoroka kutoka kituoni hapo. Wahudumu wa pale kituoni walitishia kumkataa kabisa Kassim kwa usumbufu huo wake. Msimulizi anaeleza kuwa Rehema aliwarai kwa pesa ili wamkubali tena (uk 102).

Subira ni mhusika anayetumiwa na msimulizi kudhihirisha ubwanyenye na utabaka vilevile. Subira aliishi katika mtaa wa mabanda wa Likoni akiwa na wenzake akina Riziki, Kidawa na Mwadime. Hata hivyo msimulizi anaeleza kuwa alihamia katika mtaa wa juu wa Amsterdam. Alifanya hivi baada ya mwanawe kwa jina Rukia kwenda Uarabuni na kupata pesa za kumsaidia mamake. Msimulizi anatudokezea kuwa alimshukuru Maulana kwa kumpiga kurunzi akaenda mtaa wa juu ulioitwa Amsterdam ambako alipanga nyumba aliyolipia shilingi elfu thelathini kwa mwezi. Nyumba hiyo ya Amsterdam ilizungukwa na Miasumini. Mtende mmoja mrefu, uliokuwa unakauka majani yake polepole, ulisimama mbele ya nyumba hiyo. Naye Rukia alimtilia mamake kila starehe katika nyumba hiyo. Alimnunulia friji la milango miwili na redio kubwa ya kumwongoa kwa muziki akitaka (uk 13).

Hivyo ndivyo maisha ya Subira yalivyobadilika mara moja na kuingia katika maisha mengine ya hali ya juu. Hangeweza kamwe kuishi mahali palepale katika vibanda vibovu vilivyotumiwa na walalahoi na watu masikini. Lazima angeugura mtaa huu akaishi na mabwanyenye kama yeye maadamu sasa alikuwa navyo. Alipokuwa akiuhama mtaa huo wa mabanda, aliwaachia wenzake vyombo vyake alivyoviona kuwa vibaya sasa. Kidawa alipewa kimeza kidogo kibovu cha zamani. Riziki naye akapewa vikochi viwili vilivyochoka na pipa la plastiki la maji. Subira hakutaka kugura navyo. Aliingia katika ulimwengu wa pili, kama alivyosema. Alibadili nguo zake na hata jozi za viatu mara mbili kwa siku. Mkononi alifunga saa ya bei iliyong`aa kama jua ( uk 13 – 14).

Maelezo haya yanatuonyesha hali ya mwanzo ya Subira alipokuwa katika uchochole na ukabwela wake na wenzake huko Likoni. Ni masimulizi ya mwandishi

yanayothihirisha kuwa utabaka ulikuweko katika jamii ya akina Subira, Rehema, Riziki, Mwamba na Mwadime. Mitaa ya aina mbili ilikuwepo, ile ya wachochole na walalahoi na ya walalaheri au mabwanyenye walioishi mitaa ya juu.

Vijana wengi kutoka katika mataifa mengi waliajiriwa kazi za nyumbani katika mataifa ya Ughaibuni hususan Saudi Arabia. Huko Ughaibuni, sawa na mataifa mengine, waliangukia katika mikono ya watu matajiri. Mfano wa matajiri wakubwa waliomwajiri kazi Kudra ni Bw. Aminii na mkewe aliyeitwa Nayrat. Hawa waliishi Saudia katika eneo la Arfar. Pindi baada ya Kudra kushuka katika uwanja wa ndege wa Saudia, wenyeji wake wote wawili walimchukua kwa gari aina ya Landrover Discovery iliyoenda kwa kasi kama farasi kwenye barabara ya lami iliyoundwa vizuri (uk 68).

Gari linalotajwa na msimulizi kuwa ndilo lililotumiwa na wenyeji wa Kudra kumchukua pale katika uwanja wa ndege wa Dubai, lilikuwa ni gari la kifahari na ghali na ambalo halingemilikiwa na raiya wa kawaida. Hili ni aina ya gari lililoashiria utajiri na ukwasi mkubwa. Aminii na mkewe Nayrat walipotembelewa na dadake Nayrat Bi. Fatila na mumewe Bw. Suleiman, walibebwa kwa gari jingine la Aminii aina ya Mercedes Benz la rangi ya kijivu.

Masimulizi haya yanatudokezea kuwa Bw. Aminii na mkewe walikuwa ni watu matajiri kwa kuwa na magari mawili ya kifahari. Tunafahamishwa na msimulizi vilevile kuwa waliishi katika jengo la ghorofa ambapo nyumba yao ilikuwa ni katika ghorofa ya pili nao wakaazi wa pale walitumia lifti. Zaidi na hayo, msanii anatueleza kuhusu chumba cha Aminii. Anaeleza kuwa kila chumba kilikuwa na televisheni yake na kitanda cha kisasa na meza ya kustaajabisha kwa ukubwa na urembo wake vilevile. Anasema katika nyumba hii, kila chumba kilikuwa na feni zilizofanya vyumba hivyo kuwa na hali tulivu ya hewa. Anasema sebuleni alimokaa, mlikuwa na kabati la bei na viti vya ngozi vilivyoagizwa kutoka Ulaya. Meza za sebuleni zilikuwa za glasi na zilikuwa zimeagizwa kutoka Ulaya vilevile (uk 115-116).

Maelezo haya yanadhihirisha jinsi Aminii na mkewe Bi. Nayrat walivyokuwa mabwanyenye wakubwa hapo Dubai. Waliishi maisha ya starehe hasa tunapoangalia jinsi walivyokuwa na vyombo vya bei ghali vilivyoipamba sebule yao. Walikuwa

ndio waajiri wa kwanza wa Kudra, kijana msichana kutoka Mombasa aliyenadiwa kwao na wakala tajiri aliyeitwa Rehema vilevile kutoka Kenya kule Mombasa.

Salim alikuwa ni tajiri mkubwa mjini Dubai na mwajiri wa pili wa Kudra baada ya Kudra kutoroka kutoka kwa mwajiri wake wa kwanza Aminii na mkewe Bi. Nayrat, kwa sababu ya kukatwa mshahara wake na dhuluma za mapenzi kutoka kwa Aminii. Uwezo wake mkubwa wa kiuchumi unadhihirika waziwazi. Alikuwa na hospitali yake mjini Dubai. Hii ndiyo iliyokuwa hospitali maarufu katika mji mzima wa Dubai. Hospitali yenyewe ilikuwa na madaktari kumi na wauguzi wapatao arubaini. Mwandishi anasema kuwa mji wa Salim uliitwa Paradiso. Ulikuwa Madinna. Ulikuwa na kila aina ya starehe. Licha ya nyumba kubwa, Salim alikuwa na kidimbwi cha kuogelea; kikubwa na cha kuvutia. Nyumba yake nayo ilikuwa nyumba kubwa kama kasri la ndotoni. Hapo hapo, alikuwa na sehemu ya ranchi ambako alifuga farasi, pundamilia, ng’ombe na swara. Ranchi hii ilisimamiwa na wafanyakazi wawili wa asili ya Tanzania. Hakuwa na tatizo lolote katika kulipa mishahara kwani alikuwa na hela nyingi kweli ( uk 124- 126).

Kwa mujibu wa msanii, huu ulikuwa ni utajiri mkubwa aliokuwa nao Salim huko Dubai. Alioa hapo mwanzo lakini wakaachana na mkewe akiwa masomoni ng’ambo na kumwachia binti mmoja tu. Baada ya kuachana na mkewe, hakupata kuoa tena jambo linaloshangaza kwa mtu tajiri kama yeye kuishi bila mke na mali yote hiyo aliyokuwa nayo. Kudra mfanyakazi wake aliuliza, `mtu kama Salim na hizo pesa zote alikosa nini?’ (uk 131 ).

Fauziya alikuwa ni mjane bwanyenye na ndiye aliyemwajiri Kudra baada ya kutoka katika makao ya wazee yaliyokuwa katika Jengo lililoitwa The Home For The Old. Alikuwa na watoto lakini waliokuwa na mababa tofauti. Fauziya alikuwa na rafiki wa kiume aliyeitwa Bw. Hashish naye alikuja pale kwa Fauziya mara chache kumwona. Fauziya alikuwa ni tajiri mkubwa mjini Dubai. Alikuwa na magari ya usafiri, nyumba za kukodisha na shule ya kufundisha mambo ya tarakilishi mjini Dubai. Alikuwa pia na biashara ya kukanda watu viungo vya mwili iliyoitwa Massage Parlour na wafanyakazi wapatao arubaini; wote walikuwa wasichana (uk 157- 163).

Kwa jumla vijana wanaishi na kutangamana na watu matajiri kupindukia wakati wao wenyewe ni maskini tena bila kuwa na ajira. Bila shaka vijana hupata maswali mengi juu ya utajiri wa aina hiyo ambao una watu wachache katika jamii zao. Tatizo la ukosefu wa kazi limekuwa ni donda sugu katika mataifa mengi. Hili ni tatizo linalotishia kuangamiza kizazi kizima katika mataifa haya. Hivyo basi vijana hawana budi kufanya vyovyote mradi waweze kujipatia mahitaji yao ya kila siku. Wengine wanapopata ajira za nyumbani, wengine wameingilia kazi ya usambazaji wa mihadarati, uzinzi na ulevi wa kupindukia. Baadhi ya vijana wanakimbilia mataifa ya Ughaibuni hususan Saudi Arabia ambako wanaajiriwa kazi za nyumbani. Huko Ughaibuni wanakopata kazi za nyumbani, wanakumbana na mazingira magumu ya kazi na hasa dhuluma kutoka kwa waajiri wao.

### 2. 4 Matumizi ya madawa ya kulevya

Suala la madawa ya kulevya limetawala maudhui kwa kiasi kikubwa katika riwaya ya *Pendo la Karaha.* Mwandishi wa riwaya hii anadhihirisha wazi kuwa ulanguzi wa mihadarati unaongozwa na matajiri na watu wa kutajika kwa hali na mali. Hili ni kundi lililofanya kila liloweza na lililokuwa katika uwezo wake ili kudumisha biashara hii. Kundi hili lilisambaza dawa hizi kwa siri kubwa. Liliwatumia vijana katika kusambaza dawa hizo baada ya kuwafanya wao viumbe duni. Hili ni kundi lililokuwa radhi kuondoa uhai wa yeyote aliyejaribu kulipinga katika shughuli zake.

Mzee Sanga alikuwa ni babake Kudra na aliyeuawa na kundi hili ingawa kulikuwepo na uvumi kuwa aliuawa na genge lililojiita Kuklax Klan hapo Mombasa. Watu walipozungumzia genge hilo, walisema kwa sauti za chini kwa kuwa hawakuwa na ukweli kulihusu. Lingelimtaka mtu kwa jambo lolote, lingempata. Hakuna aliyewaona wala kuwajua kwa yakini wanachama wake. Waliodhubutu kupanua vinywa vyao na kusema lolote kuhusu dawa za kulevya, walibinginywa ushahidi usipatikane. Mfano mwingine hapa ni Dhahabu aliyejaribu kutoka. Alifungua kinywa chake na aliposema alilosema, aliviziwa barabarani papo hapo na akauawa (uk 37). Hata nao walinda usalama walijifunza kushughulika na kazi zao zingine, lakini si suala la kokeini au ‘unga’ (Uk 9-10).

Baadhi ya watu walionekana kutajirika kwa haraka sana jambo ambalo lingetiliwa shaka. Watu hawa walisema mbele ya wengine kuwa wao walifanya kazi kwa bidii na kuwa ndiyo iliyokuwa sababu ya maendeleo yao makubwa. Msimulizi anaeleza kuwa mzee Sanga aliwaona watu wakiendesha magari ya bei. Aliwaona watu wakijenga mitaa yakifahari na kujipiga vifua kuwa ni watu wa mipango na miradi. Lakini alijua vizuri kuwa hao ndio waliokuwa washirika wa dawa sugu. Alisema Waliingiza hata serikali ndani ya mitandao yao ya dawa za kulevya. Walijulikana Uropa, Marekani, India na kwingine kote ulimwenguni (uk 11-12).

Hii ina maana kwamba kundi lililojishughulisha na dawa haramu lilizidi uwezo wa serikali ya nchi. Kundi ambalo lilijulikana hadi nje ya nchi yake, lazima lilijulikana na serikali ya nchi yake yenyewe. Hili ni jambo linaloweza kufanya raia wa nchi yoyote ile kuitilia shaka serikali yao. Viongozi wanaostahili kulinda raia wao na hasa vijana dhidi ya uharibifu mkubwa unaoletwa na dawa za kulevya walishindwa kulikomesha. Hii ni kauli ya kweli kwamba walanguzi wa dawa za kulevya walikuwa ni matajiri wakubwa nao waliwatumia vijana katika kusambaza madawa hayo. Wakawatumia vijana kwa kuwadanganya kuwa wangepata utajiri mkubwa. Wakaingia kwa kuahidiwa utajiri; magari, nyumba, ploti za ufuoni na vitu vingine vya starehe. Siku moja Lindo alimweleza Kudra kuwa alitaka kutoka katika utumwa huo kwa sababu alikuwa akiwatajirisha watu wengine walioendesha Mavolvo, Mercedes Benz, Malandrovers, Discovery na yeye mwenyewe ni mtumwa. Hakulala kisa na maana ni kuzungusha dawa angalau kumlipa mkubwa wake (Uk 31). Janette akipigana na nafsi yake alipokuwa katika mawazo makubwa aliiambia nafsi hiyo isimkere kwa kuwa yeye alikuwa ni mtumishi. Akataka nafsi hiyo imuulize Bilali kwani ndiye mwenye biashara hiyo na kwamba wao walikuwa ni wajakazi tu. Hata hawakupata faida yoyote (uk 37).

Vijana walijuta kuingia katika mtego huo wa dawa za kulevya. Wengi walishindwa kujinasua hata baada ya kufahamu kwamba waliwatajirisha watu wengine. Vijana hawa waliwekewa kila mmoja ‘ration’ yake ya kusambaza kila siku. Lindo alipotaka kujua alikokua Regina aliambiwa bado alikuwa akizungusha kasma yake kwa sababu alikuwa amechelewa kuamka, wakati yeye Lindo alfajiri alikuwa barabarani amekwisha sambaza `ration’ yake na kumpa Wambui pesa zenyewe (Uk 34).

Hii ni jamii iliyojengwa kwa kuwepo matajiri wakubwa. Waliwaajiri vijana kuzungusha dawa zilizowaletea pesa nyingi kupindukia. Vijana walilazimika kujizatiti mapema kwa kuwa waliwekewa kila mmoja kiwango chake ili nao wapate malipo yao. Matajiri hawa hawakujali hali ya maisha ya vijana hawa mradi wao wenyewe wapate pesa kutokana na dawa zilizouzwa. Namna walivyotajirika kwa kasi ni suala lililowashangaza wengi katika jamii hii.

## 2. 5 Dhiki za ajira ng`ambo

Kudra ni kijana wa kike aliyesafiri hadi Uarabuni kule Saudia ili kutafuta riziki yake ili aweze kumsaidia mamake Bi. Riziki ambaye alikuwa mjane. Alilakiwa vyema sana na wenyeji wake, Aminii na mkewe Bi. Nayrat. Hawakuonekana watu wabaya mwanzoni. Bi. Nayrat alimpa Kudra simu ili amjulie hali mamake akiwa nchini Kenya huko Mombasa. Ukarimu huu haukuendelea kwa muda mrefu kwani Bi. Nayrat alianza kutoa visababu vya kukosa kumpa simu ampigie mamake ambaye alikuwa akiugua. Nayrat akakosa huruma kwa mfanyakazi wake aliyesafiri kutoka mbali nchini Kenya na aliyemwacha mamake akiwa katika hali mbaya ya afya. Vile vile alikosa kutambua kuwa huyu ndiye aliyekuwa mwana wa pekee na aliyetegemewa na mamake. Bi. Nayrat alimkataza hata ruhusa ya kutoka nje kukutana na watu au vijana wengine alipokuwa hana kazi ya kufanya. Haya yanadhihirisha wazi kuwa mwajiri huyu alikosa kufahamu kuwa binadamu hukamilika kwa kuingiliana na kutangamana na binadamu wenzake na kwamba hata mfanyakazi ana uhuru wake.

Mshahara walioahidiana haukulipwa wote kwa mfanyakazi huyu. Alimwamsha mapema kwa kengele na hata akapata matusi kwa kuitwa kelbu. Miezi ikapita hata senti moja hakupata ila chakula cha makombo baada ya wao kula (uk 87-93). Vitendo vya mwajiri huyu wa Kudra vyaonyesha dhuluma kubwa kwa mtumishi wao. Msimulizi anatueleza kuwa hata walimshonea nguo maalumu ya kumtambulisha akiwa kazini. Waajiri hawa walijua kuwa Kudra alikuwa ameteseka vya kutosha na wakajua kuwa angetoroka. Walianza kumtolea vitisho kuwa akijaribu kutoroka watamlimbikizia makosa ili aozee katika jela huko Dubai. Nayrat naye alifika kima cha kuanza kumpiga Kudra. Alianza kwa kumrushia vitu Kama vikombe alipokosa. Sasa alimzaba makofi na kumpiga kwa fimbo (Uk 105).

Tunadhihirishiwa na msanii jinsi dhuluma ya mwajiri wa Kudra ilivyozidi. Hata Kudra alipougua, mwajiri hakuonyesha huruma kwa kijakazi wao aliyewatendea kila aina ya kazi pale kwao. Jioni moja alikuwa hajisikii vizuri. Licha ya kumweleza Nayrat hali yake, hakutaka kuzingatia lolote. Alifanya kazi hadi Nayrat mwenyewe akaona kuwa hawezi kufanya kazi kikamilifu. Alilofanya ni kumwita *"lazy woman*"na kumwambia akalale.

Yote haya yanadhihirisha kwamba hawakumjali kijakazi wao kwa lolote lile. Mwandishi anatueleza kuwa Kudra alifanyishwa kazi hata alipoamka asubuhi hakuwa amekitandika kitanda chake kwa ajili ya haraka aliyokuwa nayo. Walimkosea heshima na kumwona kama chombo kisichostahili kutambulika. Nyumbani hapo alimokaa, walimwona kama kinyesi cha mbwa (uk 107).

Baada ya kutoroka kazi kwa Salim, Kudra alipata kuajiriwa kazi ya nyumbani kwa Bi. Fauziya, bwanyenye mjane mjini Dubai. Baada ya kufanya kazi kwa siku chache pale nyumbani, Fauziya alimweleza Kudra kuwa alikuwa na kazi nyingine nje kidogo ya mji wa Dubai na kwamba kazi hiyo ingempa pesa zaidi. Kazi hiyo ilikuwa katika jumba aliloliita Massage Parlour nayo ilihusu kuwakanda watu viungo vya mwili. Akaambiwa nikazi ya kuwafurahisha wateja. Wakitaka muda zaidi wa kukandwa, humlipa mkandaji (uk162).

Kudra alipotoroka kazi kwa Bw. Aminii na Nayrat pale Arfar, alipata ajira nyingine kwa Bw. Salim. Salim aliishi yeye na bintiye wa pekee kwa jina Hanawi aliyeachwa na mamake akiwa na umri mdogo baada ya ndoa ya Salim na Salma kuvunjika. Mwandishi anaeleza kuwa Salim hakupata kuoa tena licha ya kuwa alikuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Alikuwa na mali nyingi na wafanyakazi wa kutosha kama vile hospitalini kwake, mochari, walinzi wawili langoni nyumbani kwake na vijana wawili katika ranchi yake. Salim alimdhulumu Kudra kimapenzi kwa kutaka kumtumia Kudra tu. Hii ni kwa kuwa alitaka jambo hilo libakie kuwa siri kubwa baina yao wawili na kwamba bintiye Hanawi asijue licha ya kuwa Hanawi alikuwa ni mtu mzima na uhuru wake. Siku moja usiku, Kudra alipokuwa amelala, alisikia mlango wa chumba chake ukigongwa. Mgoto uliendelea hata ukamwamsha. Aliangalia saa yake ya mkononi, ulikuwa usiku wa manane. Alipofungua mlango, alimwona Salim amesimama hapo. Alikuwa hasemi lolote ila kutabasamu tu. Akaona amwachie

mkubwa wake aseme mwanzo. Alitamka maneno matatu tu ya “I love you” ambayo Kudra alisema yalikuwa mazito kwake.  Maneno yaliyoonyesha kuwa Salim alitaka uhusiano wa mapenzi baina yake na mwajiriwa wake (uk 131-132).

Huu wote ulikuwa ni mchezo wa kumchezea Kudra. Wafanyakazi wengine pale kwa Salim walimweleza Kudra kuwa Salim alizoea kuwaleta wasichana pale akiwatumia na mwishowe akiwafukuza. Dele na Kele walikuwa ni vijana wa kiume walioajiriwa kazi na Salim ya kuwalisha na kuwatunza farasi pale katika ranchi yake. Vilevile ndio waliokuwa walinzi wa wanyama wengine pale katika ranchi ya Salim kama vile pundamilia, ngamia na swara. Dele na Kele walitoka Kenya sehemu ya Shimo la Tewa. Vijana hawa walikaa hapo kazini kwa Salim kwa miaka mingi na hawakupewa ruhusa ya kwenda nyumbani au kuwajulia hali wazazi wao. Mwandishi anasema kuwa Dele hakupewa nafasi ya kwenda kumzika babake, akawa anamwomboleza papo hapo kazini (uk 149). Siku moja Kudra alimweleza Dele kuwa hangemlegeza Salim na kwamba pale kwa Salim palikuwa sasa ni kama kwake, Dele alishangazwa sana naye.

Mshangao huu wa Dele unaonyesha kuwa alimhurumia na kumwajabia Kudra aliyekuja pale siku chache na bila ya kupaelewa mahali hapo vizuri, alidai sasa ni sawa na kwake. Dele alimcheka Kudra kwa kuwa hakumwelewa huyo Salim na mchezo wake wa kuwachezea wasichana. Ushahidi mwingine ni kwamba siku moja tu baada ya Kudra kuondoka pale kwa Bw. Salim, jirani yake, Suzana alimweleza kuwa msichana mwingine alikwishaingia pale kuchukua nafasi yake. Kudra hakuamini kuwa Jana alikuwepo, leo mwingine yupo (uk148). Kwa jumla vijana wanajikuta katika jamii yenye watu matajiri. Hawa wanawathulumu kwa mishahara midogo na kazi nyingi kupindukia.  Wanathulumiwa kimapenzi kwa sababu wako pale kuwarithisha mabosi wao wanaowatumia vibaya.

Mazungumzo kati ya Kudra na Fauziya yanadhihirisha kuwa mbali na kazi ya ukandaji miili iliyofanywa pale, yeye mwenyewe Fauziya aliruhusu wafanyakazi wake kufanya biashara yao na wanaume iliyohusu kuonana kimwili. Bila shaka Fauziya aliwatumia wafanyakazi wake katika biashara ya ngono kama chambo cha kuwaleta wanaume pale ili wakandwe miili na mwishowe kumwachia Fauziya pesa nyingi. Huu vile vile ni mfano wa dhuluma kwa vijana wa kike wanayofanyiwa na

waajiri wao. Kudra alipojarbu kuikataa kazi ile ya ukandaji miili alilazimishwa kuifanya. Msimamizi wa kazi ile aliyeitwa Saumu alimweleza angemlazimisha aifanye. Dhuluma ya kulazimishwa kuifanya kazi ambayo hakuipenda na kupigwa vita kama namna ya kumshurutisha aifanye ndiyo iliyokuwa hali ya maisha ya Kudra pale kwa Fauziya. Siku moja alipokuwa hali, Saumu alimwita, akampiga makofi na viboko. Kudra naye alikaa akitafuta mwanya wa kutoroka. Katika muda wote aliokaa, Saumu alimpiga mara saba, hata siku moja akamvunja mkono. Fauziya naye alikuwa nadra kuja na alipokuja ilkuwa haramu kusema naye. Wasichana waliojaribu kusema naye, baadaye walipigwa na Saumu na Walinzi wa pale *massage Parlour* (uk 166).

**2. 6 Kutowajibika kwa Serikali**

Kiongozi ni mtu anayewasimamia na kuwaelekeza watu au kikundi cha watu (wanajamii) ili wafanye kazi au shughuli za kuwaendeleza kwa njia inayostahili. Kwa ufupi kiongozi huwaongoza watu katika kutenda mema kwa njia ya haki na kuridhisha. Katika *Vipanya vya Maabara* (2007) na *Majira ya Tufani* (2012*),* Njoroge (2014) anasema tuna aina tofauti za viongozi. Tuna viongozi wa serikali, wabunge, wazazi wa kiume na vile vile wa kike baina ya wengine. Jamii ya *Pendo la Karaha* ni jamii inayotawaliwa na viongozi wabaya. Hili linadhihirika kupitia mhusika Jannete anayehojiana na nafsi yake mwenyewe juu ya viongozi. Nafsi yake inamwonyesha kuwa yuko katika utumwa mkubwa wa uraibu wamatumizi ya dawa za kulevya. Anaiambia nafsi yake kuwa huu si utumwa ila ni jambo la hiari. Kisha anaiuliza nafsi yake kwa nini isiwaulize wale viongozi waibao mapesa watoke kwenye utumwa huo. Haya yanaonyesha wazi kuwa viongozi walioko ni viongozi wezi. Mwamba aliitoa kauli kama hiyo hiyo aliposhambuliwa na kidawa akilaumiwa kuwa ni yeye Mwamba aliyesababisha kifo cha Lindo mwanawe Bi. Kidawa. Alimwambia Kidawa kuwa hao waliowasukuma watoto wao kwenye dawa ni hao matajiri na viongozi wao. Wanawachagua wao wenyewe na wanawafanya wabunge kwa kura zao na wengine wakiwafanya madisii.

Kauli hii ya Mwamba inaweka mambo wazi kuwa baadhi ya viongozi ni waovu ingawa viongozi hao wanawekwa mamlakani na wale wanaowachagua kwa njia ya kuwapigia kura. Huu ni mfano wa tatizo lililoko katika mataifa mengi linalohusu uongozi mbaya bila ya jamii kufahamikiwa kuwa jamii iyo hiyo ndiyo chanzo hasa

cha uongozi wa aina hiyo. Bi. Kidawa na Bi. Riziki wanapozungumzia matatizo yanayowakumba, wanaelekea kulionyeshea kidole bara la Afrika kuwa limelaaniwa. Wanasema kila wakipata chao mkononi, yuko huyu kucheza nao. Riziki anaposema hii ni laana, anaambiwa na Kidawa kuwa si laana ila ni uongozi wao. Kwamba jambo dogo tu la dawa Mombasa lilishinda serikali kwa kuwa kila mmoja ni mhusika katika njia fulani (uk 123). Wanashindwa ni kiongozi yupi anayestahili kujulishwa tatizo hili kwa kuwa wote ni wahusika kwa njia moja au nyingine. Mwandishi anakielezea kijiji cha Baghdad kama kijiji kilicho laaniwa na kilichokaa watu wa uraibu wa dawa za kulevya. Anaeleza kwamba hii ilikuwa ni sehemu ambayo ilikuwa nje ya nchi ya Kenya. Msanii anasema Baghdad ilikuwa mtoni hasa. Wenyewe wakakiita Ughaibuni maana hawakuona ni sehemu ya nchi ya Kenya. Hakukuenda mtu wa jina na maana. Hata polisi hawakwenda.

Hii inakuwa ni kinaya kikubwa kuamini kuwa kulikuwa na sehemu yoyote ya nchi ambayo haikujulikana na viongozi wa nchi wakiwemo polisi. Askari ambao wamepewa majukumu ya kulinda usalama na kuhakikisha utangamano katika jamii vile vile ni viongozi katika jamii hiyo. Hutoa mawaidha na kuilekeza jamii katika njia inayoweza kuleta amani na utangamano mzuri. Baadhi ya shughuli zao ni kutangamana na jamii katika maeneo yake ya makazi katika juhudi za kuwahakikishia usalama wao. Hivyo basi askari walitarajiwa kuielewa na kuitembelea sehemu nzima ya Baghdad. Hii ilikuwa ni sehemu ambapo kila aina ya bishara ilifanyika. Mwandishi anasema kuwa kama si kuuza kaimati ni biashara ya pombe. Kama si pombe, ni biashara ya nguo mbovu. Kama si biashara ya kuuza mitura ya walevi, ni biashara ya mchuzi. Anasema Baghdad kuliuzwa kokuteli, unga na hata gomba. Walioifahamu Baghdad pia waliita Gomora. Ilikuwa ‘nchi’ kivyake. Hata walikuwa na ‘rais’ wao na hata ‘baraza lao la mawaziri’. Vile vile walikuwa na ‘Bunge’ lao lililojadili mustakabali wa ‘nchi’ yao, yaani Baghdad. Mtu aliweza kuzaliwa Baghdad na afe hajaingia Mombasa mjini. Atakwenda kufanya nini Mombasa? Kila haja yao ilitimizwa hapo Baghdad. Anasema hiki kilikuwa kijiji cha kuogofya na kutisha. Kilijaa kila aina ya dawa za kulevya na uraibu. Kama si pombe ni mairungi. Kama si unga, ni bangi. Kama si kokeini, ni sonyo (uk 40).

Hii ni sehemu ambayo bila shaka ingejulikana na viongozi na mtu yeyote yule katika maeneo ya karibu. Haiyamkiniki kwamba polisi kama viongozi hawakuijua sehemu ya Baghdad kwa vyovyote vile. Aidha waliijua sehemu hii na biashara yake wakachukua hongo na kuifumbia jicho sehemu yote hiyo na vituko vyake. Kikundi kilichoongoza maandamano ya kwenda kukiteketeza moto kijiji cha Baghdad kikiongozwa na Subira, Riziki, Kidawa na wanawake wengine, hatimaye kilifanikiwa kumkamata Jannete. Kikundi hicho kilirudi Mombasa mjini kikampeleka Jannete katika kituo cha polisi cha Makupa. Aliposhtakiwa hapo kituoni Makupa kuwa ni muuzaji sugu wa dawa, askari wa hapo walimfungia seli kwa muda mfupi tu kisha wakamwachilia. Mwandishi wa riwaya hii anaeleza kuwa saa kumi na moja, akawa ametoka yuu huru kama mnyama pori. Aliwacheka na kuwatukana wale waliotaka kutia kitumbua chake mchanga. (uk 42).

Mwandishi wa riwaya ya *Pendo la Karaha* anadhihirisha hali ilivyo leo katika vituo vyetu vya polisi. Mshukiwa aliyepelekwa pale alitiwa ndani kwa masaa mawili tu. Huo ulikuwa ni muda mfupi sana wa polisi wa pale kufanya uchunguzi wao wa kina na kutosheka kwamba huyu hakusambaza madawa hayo. Suala la uuzaji na usambazaji dawa hizo ni dondasugu katika mataifa mengi na linalotishia uhai wa vijana wetu. Iliwapasa kumshikilia mshukiwa Jannete kwa muda ili kumchunguza kwa kina. Badala yake, polisi wale walingojea wale waandamanaji waliomleta kutokomea kisha wakamwachilia kutoka katika seli zao hapo Makupa. Kitendo hicho cha polisi kinaonyesha kutowajibika au uzembe wao kama viongozi.

Rehema, tajiri aliyewasafirisha vijana Ughaibuni kwa manufaa yake mwenyewe, ni mfano mwingine wa mtu aliyefumbiwa macho na serikali licha ya serikali na viongozi kwa jumla kuifahamu biashara yake kule Changamwe. Mwandishi anasema kuwa Rehema alikuwa na ofisi kwenye njia ya Haile Selassie katika jengo la Monitor. Hapo wasichana wengi kutoka Kisumu, Nairobi, Nakuru, Mombasa na kuingineko walifika ili kunaadiwa na kusafirishwa hadi mataifa ya kigeni. Mwandishi anasema kuwa Kudra alipofika kwa Rehema kutafuta usaidizi wa kusafiri Ughaibuni, alipewa kijitabu cheusi kilichokuwa na majina ya vijana waliojitokeza. Aliwaona waliotaka kwenda Lebanon, wengine Dubai na wengine Saudia. Aliwaona pia wengine waliotaka kwenda Uropa, Marekani na wengine Pakistani. Yeye alikuwa msichana wa elfu moja katika orodha hiyo (uk 25).

Haya yanaonyesha kuwa Rehema alikuwa ni wakala mkubwa katika eneo lote la Mombasa na alikuwa amewanasa wasichana wengi sana. Kwa kazi hii, alipata mshahara wake kwa makubaliano waliowekeana. Alicheka huku Subira akilia. Alijijali yeye mwenyewe mradi apate mgao wake. Hakujali kilichowapata wazazi wa hao vijana aliowapandisha ndege wala kile ambacho kingewapata Ughaibuni baadaye. Hii ni biashara ambayo serikali na viongozi wengine hawangedai kutoijua kamwe. Mwandishi anasema Rehema alijenga nyumba mtaa mzima wa changamwe kwa kunadi vijana Ughaibuni. Alinunua mabasi yakapewa jina ‘maisha ni hiari yako’. Serikali nayo ikamfumbia jicho. Haikujali kwamba vinywa vya watu vililalamika. Magazeti yalilalamika lakini Rehema alitembea Changamwe kwa madaha akisuta maadui wake kwa kiburi (uk 56). Yeye mwenyewe hakujali chochote kwa sababu alijua alilindwa na serikali na viongozi katika eneo lake. Suala la kuwa serikali ilifahamu yale yaliyokuwa yakitokea nchini na hata yaliyowapata vijana Ughaibuni, ni suala lisiloweza kufichika. Kauli iliyotolewa na Kudra alipokuwa katika foleni ya kujiandikisha ili kurudi nyumbani Kenya, inadhihirisha hilo. Alijiuliza: ``Kwa nini serikali haikulazimisha nchi kama hizi kuwalipa wasichaana hawa kama walivyokubaliana? Hivi serikali haikujali kama waliishi au la? Mbona serikali inasema jukumu la kulinda haki za raia ni lao?” Kudra akaona kuwa mikataba walioandikiana Dubai ikawa ni mambo ya kuchekesha tu. Ilipuuzwa, ilibezwa (uk176).

Kauli hii inaonyesha kuwa nchi zote zilizohusika kuwapokea vijana kutoka katika mataifa mengi ya Afrika, zilikuwa zimewekeana makubaliano fulani juu ya kazi zao Ughaibuni na ulinzi wao wanapokuwa huko. Hili linaonekana kuwa halikutiliwa maanani kwa vyovyote. Uzembe na utepetevu wa serikali haukuwa ni tatizo la viongozi katika Afrika pekee. Tatizo hili linakuwepo pia katika mataifa ya Ughaibuni ambako vijana walikimbilia kutafuta mustakabali wao. Kudra alijaribu kutafuta majibu kwa maswali mengi kama ni vipi vijana wangefanyizwa kazi tofauti na zile walizokwenda kufanya Dubai na madhila mengi waliyotendewa na waajiri huku serikali wakiwemo polisi wasijue kilio chao. Kudra hakuelewa ni vipi mambo yale yangetokea katika mji wa Dubai bila ya serikali kujua. Alishindwa Polisi wa Dubai walikokuwa. Baadaye, alikuja kuelewa kuwa askari, baada ya kupewa hongo na Fauziya, hawangefanya jambo lolote au kumsikiliza yeyote (uk 168).

Hata baada ya habari ya masaibu ya vijana kule Dubai na Saudia kujulikana na viongozi mbalimbali katika mataifa wanakotoka, serikali zilizembea katika kuchukua hatua mwafaka na za dharura ili kuweza kuwanasua. Kulingana na mwandishi tatizo kama hili liliangaziwa kwa kina na vyombo vya habari yakiwemo magazeti ya nchini Kenya na kuishia kujadiliwa bungeni. Viongozi hawa katika bunge la taifa walinyoshea kidole serikali kwa jumla kwa kuzembea katika suala hilo. Kiongozi na waziri mmoja aliyesimamia masuala ya wanyama aliuliza kama Afrika ilikuwa inapelekwa tena katika jinamizi la utumwa na ukoloni. Aliwauliza wenzake bungeni ingwezekanaje habari hizo zinapokuja, serikali haifanyi jambo lolote? Kwamba na wao waliendelea kustarehe huku vijana wakinyanyaswa. Akasema bungeni kuwa vijana wengine hufukuzwa kazi wakaishia barabarani. Alimweleza spika maoni yake kuwa aliona serikali ilizembea jukumu lake (uk 171 – 172). Hii inaonyesha wazi kwamba viongozi barani Afrika wanafahamikiwa na suala hili wala hawachukui hatua yoyote. Matukio kama hayo katika jamii ndiyo yanayowafanya vijana wetu kukata tamaa maishani na kujikuta katika hali mbalimbali katika juhudi zao za kujiendeleza.

## 2 . 7 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia jamii ya *Pendo la Karaha*. Tumefanya hivyo kwa njia ya kuitathmini jamii hii kutokana na kuelekezwa na kuongozwa na nadharia yetu ya Uhalisia Hakiki. Hivyo basi tathmini ya jamii hii ni suala ambalo halingeepukika kwa sababu jamii ndiyo ambayo inaelekeza vijana wetu katika nafasi mbalimbali ambazo wanajikuta, chanya na hasi vilevile. Tathmini hii imeongozwa na kiunzi cha tatu cha nadharia ya Uhalisia Hakiki kinachodai kuwa matukio katika jamii hutendeka kwa kusababishwa na masuala mbalimbali. Sura hii imetutayarisha katika kuziangalia nafasi za vijana katika kazi itakayofuata.

Baadhi ya masuala yaliyojitokeza ni ukabwela au uchochole mkubwa unaoikumba jamii hii, mitaa ya mabanda na hali duni ya maisha. Utajiri mkubwa vilevile umedhihirika na kwa jumla utabaka kwa kuwepo mitaa ya juu. Usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya unaoongozwa na matajiri kwa kuwatumia vijana wasio na ajira katika jamii. Limejitokeza suala la ukandamizaji na dhuluma kutoka kwa waajiri kwa namna mbalimbali zikiwemo dhuluma za mapenzi na za kiuchumi kama baadhi ya changamoto zinazoikumba jamii hii ya vijana. Aidha hii ni jamii

inayoongozwa na viongozi wasiojali masilahi ya watu wake na hasa vijana kwa kuzembea katika majukumu yake. Vijana wanaposahauliwa kwa namna ilivyojitokeza, hawana budi kujitafutia maisha na mustakabali wao kwa namna mbalimbali.

# SURA YA TATU

## NAFASI YA VIJANA KATIKA *PENDO LA KARAHA*

### 3. 1 Utangulizi

Majukumu ya vijana katika jamii yamekuwa yakibadilika jinsi hali ya jamii inavyoendelea kubadilika vilevile. Katika mfumo wa maisha ya kiasili ya Mwafrika kabla ya maajilio ya wageni na elimu ya Kimagharibi, malezi ya vijana pamoja na kuwaelekeza katika jamii yalikuwa ni wajibu wa jamii nzima. Tabia potovu miongoni mwa vijana zilishtumiwa na watu wote kwa vile maisha yalikuwa ni ubia au ushirika. Watoto walikuwa chini ya jicho pekuzi la jamii nzima kila wakati. Majukumu ya vijana vivyo hivyo yalikuwa bayana huku vijana wa kiume wakiandamana na wazazi wao katika shughuli kama uwindaji na jinsi ya kuihami jamii na baadaye kuzikidhia familia zao walipooa. Wasichana nao walifundishwa mambo ya unyago yaliyozingatia utekelezaji kamilifu wa majukumu yao wakishaolewa. Katika hali hii ya maisha ya kitamaduni, vijana hawakuwa na changamoto nyingi kwa sababu kulikuwa na utaratibu wakuwaeleza kulingana na kila jamii, Erikson (1961).

Leo hii mambo yamebadilika si haba. Swala la malezi ya watoto na vijana limekuwa ni jukumu la mzazi binafsi kwa sababu hali ya maisha ya jamii imebadilika. Uchochole, ubwanyenye, ubinafsi, ukabila, utoaji rushwa, wizi wa mali ya umma na ukosefu wa ajira ni baadhi tu ya changamoto zinazoikabili jamii na hivyo kuwafanya vijana wengi kujishughulikia.

Tathmini iliyofanywa na Pawson na Tilley (2002) kuhusu Uhalisia Hakiki inadai kuwa taratibu za kufanya mambo yanayochochewa na mazingira na kutokea huleta matokeo yanayoweza kuwa ni ya kupendeza (chanya) na yasiyopendeza (hasi). Hivyo basi nafasi tunazotarajia katika sura hii ni zote, chanya na hasi.

### 3. 2 Nafasi chanya wanazopewa vijana

Mwandishi wa riwaya ya *Pendo la Karaha* amewapa vijana nafasi hii chanya katika kubainisha na hata kuchochea mwamko wa vijana. Hivyo basi wamebainishwa katika

riwaya hii kama watu wenye maadili, wenye ari ya kujikomboa na kama mihimili ya taifa katika kutaja nafasi chache.

### 3. 2. 1 Vijana na Uhuru wa mawazo

Msanii amewasawiri vijana ambao wamejikomboa kimawazo. Katika riwaya ya *Pendo la Karaha*, Kudra ana mawazo yaliyo huru na yasiyoweza kuyumbishwa ovyo. Alipoona mamake alivyoendelea kuteseka katika hali ya uchochole, alishindwa kuelewa ni vipi mamake angeweza kumtimizia mahitaji yake ya shuleni kama vile karo. Mawazo yake sasa yalikuwa ni katika kutafuta kazi ili amsaidie mamake ambaye alikuwa sasa ni mjane baada ya kufiwa na mumewe Bw. Sanga. Kudra alimjulisha mamake juu ya wazo lake la kuwacha shule. Aliona kuwa kuendelea kutafuta elimu ilikuwa sasa ni sawa na dau la mnyonge ambalo haliendi joshi au bidii isiyozaa matokeo yoyote. Mamake aliposhikilia kwamba lazima angeendelea kuwa shuleni, Kudra alikataa kwa kinywa kipana na akamwambia mamake kuwa akili zake hazikuwa katika mambo ya elimu (uk 6).

Kudra aliendelea kumshawishi mamake akubaliane na mawazo yake hasa alipompa mfano wa Subira aliyemruhusu bintiye Rukia kwenda Saudia kutafuta ajira. Alimwambia mamake kuwa Rukia tayari alikuwa amemwandikia mamake mfanyakazi wa kumsaidia. Riziki, alimwambia bintiye kuwa ni Mungu aliyewakumbuka hao. Kauli hiyo ilimfanya Kudra amwambie mamake kuwa halikuwa suala la Mungu ila ilikuwa ni juhudi zao na mipango yao vilevile.

Alipofika kwa wakala wa ajira za Uarabuni, Bi Rehema mwenyewe alimuuliza Kudra kama walikuwa wamezungumza na mamake akamkubalia. Kudra alimjibu wakala huyu kuwa yeye sasa alikuwa ni mtu mzima na kwamba angeweza kujiamulia mambo yake mwenyewe. Alimwambia Rehema ambaye ni wakala, "Mama hana neno. Mimi ni mtu mzima sasa. Ninaweza kujiamulia mambo yangu mwenyewe bila kumhusisha mamangu "(uk 24).

Maelezo hayo yanatudhihirishia kuwa vijana ni watu ambao wamefikia kiwango cha kuachwa huru ili wajiamulie mambo yao. Hii inatokana na sababu kuwa wamekosa ajira nchini na hata pale wanaposoma, asilimia fulani ya vijana hao hawanufaiki kwa

vyovyote. Baadhi yao wamewaona wenzao wakifaulu hata wanapotoka katika mikono ya wazazi wao.

Uhuru wanaotafuta vijana wetu unachochewa na hali ya kukosa matumaini hasa kutoka kwa viongozi wanaopaswa kuwashughulikia. Wanajiona kama kundi lililosahaulika na hivyo basi hawana budi kuikata minyororo inayowashikilia kwa wazazi na viongozi wao katika jamii.

**3. 2. 2 Vijana na maadili**

Vijana wamechorwa kama watu ambao ni imara katika vishawishi vinavyoweza kuwaingiza katika mitego ya uasherati. Kama hatua muhimu ambayo humtambulisha binadamu ndani ya jamii yake, msingi wa kwanza wa maadili unapatikana ndani ya familia, kwani huko ndiko mtoto anakoanza kujifunza mambo na kisha kuendelea nayo hadi mwisho wa safari yake ya maisha. Baadhi ya vijana wameyashikilia maadili yao kwa kusimama kidete dhidi ya vitendo viovu kama mapenzi ya kiholela. Kudra alisimama imara dhidi ya vishawishi vya mwajiri wake.

Huu ni msimamo uliokuwa wa kijasiri sana hasa Kudra alipokumbuka tisho la mwajiri ambalo lingemfanya afukuzwe kazi hapo kwake. Tabia ya mwajiri wa Kudra haikukoma mara ile ile alipotishiwa kusemwa kwa mkewe Nayrat. Aminii aliendelea kumshawishi Kudra amkubalie wafanye urafiki wa kimapenzi. Kudra aliushikilia msimamo wake na akamwambia kuwa yeye alikuwa ni mfanyakazi wake na tena hakutaka vita na mkewe (uk 110).

Mwajiri wa Kudra alipoona kuwa hangefaulu kabisa katika kumshawishi Kudra katika mapenzi aliyoyataka, alianza kubadili mbinu yake. Sasa alitumia vitisho kuwa angemsingizia makosa na kumfungulia mashtaka akikataa ili amfukuze au hata amwingize jela. Kudra hakujali chochote hata kama ni kutiliwa hiyo kesi. Aliona afadhali kesi lakini asimkubalie (uk 111). Huu ni msimamo kwa kijana aliyepokea mafunzo mema kutoka kwa wazazi na jamii yake.

Katika massage parlour, biashara iliyofanywa na Bi. Fauziya ilikuwa ya ukandaji viungo vya mwili. Kudra alipelekwa katika chumba kimoja ambamo wasichana wanne walimkanda mzee aliyekuwa amelala kwa kupozwa na anasa. Mwandishi

anasema mzee huyu alikuwa na kaptula tu. Kudra alionyeshwa kazi ya kufanya na ingawa aliifanya kwa uzito mwingi moyoni, hakuifanya kama walivyomweleza wale wasichana wanne. Aliporipotiwa kwa msimamizi wa pale kuwa alikataa kufanya alivyoagiza, Saumu alimwita ofisini. Kudra alimwambia waziwazi, 'mimi kazi hiyo siipendi, sitaki kuifanya.' (uk 165).

Vijana katika jamii wamechukua msimamo wao wa kujihadhari na vishawishi kama vya ngono ya kiholela ambavyo vinaletwa na wale walio katika nafasi nzuri za kiuchumi. Watu kama hao wanatumia unyonge walionao vijana ili kuwatumia katika mapenzi ambayo hayastahili.

### 3. 2. 3 Vijana na ari ya kujikomboa kiuchumi

Mwandishi amewasawiri vijana kama watu wenye uwezo wa kujikomboa kutokana na utumwa wa aina yoyote ile. Wanjiku na Akinyi (1993:1) wanapotoa pendekezo kuhusu suala la usawa wa kijinsia, wanaeleza kwamba maumbile hayawezi kubadilishwa lakini mfumo unaodhalilisha na kuwakatiza wengine tamaa ya kujiendeleza, unaweza kubadilishwa kwa sababu ni tokeo la jamii la mazoea na desturi. Kwao jamii inaweza kubadili mfumo ulioanzishwa na wanajamii wenyewe.

Msanii ametuonyesha jinsi vijana wanavyojitahidi katika kujikomboa kutoka katika changamoto za aina mbalimbali. Kudra alipotambuwa kuwa mamake ameshindwa kufanya kazi, alifikiria afungue biashara yake. Hii ni kwa sababu alikuwa amefanya kazi za mahotelini, madukani kwa wahindi na kwingineko. Mwandishi anasema Kudra aliona mshahara wa kuwa kibarua haukumtosha. Mamake alipomwuliza kama alikuwa na mtaji alimwambia hakuwa nao lakini rafiki yake angemkopesha kisha baadaye amrudishie (uk 58).

Mhusika Kudra alitafuta kazi kila mahali hapo Mombasa katika maduka na mahoteli bila kufanikiwa. Mwishowe tunaelezwa kuwa alipata kazi ya kufua nguo huko Nyali. Huko aliandamana na rafiki yake wakaenda kila siku na akalipwa shilingi mia mbili baada ya kufua nguo. Kazi hii ilimwezesha kuinua hali yake ya maisha na ya mamake. Siku moja Kudra na Zuhra wakifua nguo Nyali, Kudra alimweleza, `nimekuwa mwanamke mzima. Nitamtegemea mamangu hadi lini? Naye mamangu ni mjane. Ni mtu wa taabu. Hana uwezo' (uk 60). Alipokuwa Dubai alimtumia mamake pesa na kumhimiza aanzishe mradi wa kuku na anunue kizalio cha vifaranga.

Alipata pia mkopo wa Benki fulani ili aweze kumaliza nyumba za kukodisha alizokuwa akijenga (uk 181).

Vijana waliokuwa wameingia katika uraibu wa dawa za kulevya walijaribu juu chini kujinasua kutoka katika utumwa huo. Kassim ni mfano wao. Aliweza sasa kuisimamia kampuni ya mamake ya Rehema Logistics.

Vijana wanafanya kila juhudi za kujikomboa baada ya kugundua kwamba wao wenyewe ndio ambao wangejinasua kutoka katika jamii dhalilishi na isiyojali kesho yao. Vijana wanaofunguka macho na kuona haja ya kujianzishia miradi yao wenyewe baada ya ajira kutoka kwa serikali zao kukosa ili wajinufaishe wao na jamii zao zinazokandamizwa na mabwanyenye.

### 3. 2. 4 Vijana na majukumu ya kuwatunza wazazi

Vijana wamesawiriwa kama watu wenye kujali wazazi wao hasa wanapolemewa katika uzee na afya. Baada ya kifo cha babake Kudra, Bw. Sanga, mamake Kudra Bi. Riziki alishughulika sana ili aweze kujikimu yeye na mwanawe Kudra ambaye alikuwa angali shuleni. Kudra alimwona mamake akiuza mbaazi, maharagwe sambusa na vitumbua. Alimwona mamake akipambana na moto wa majiko huku moto huo ukimuuguza mikono na kumwachia mabaka ya alama mikononi. Tunaelezwa, `wakati fulani, alitaka hata kuondoka shuleni ili kumwondolea mama yake kero ya kulipa karo, kumnunulia vitabu ghali na hata kumnunulia sare (uk 2).

Katika siku chache alizompigia mamake simu kutoka Dubai, Kudra aligundua udhaifu aliokuwa nao mamake katika mazungumzo yake. Simu hizo zilimfanya Kudra kujua kuwa mamake alikuwa hana nguvu na kuwa labda aliugua. Kudra alimshauri mamake asiendelee na biashara hiyo ili apate muda wa kupumzika na pia atilie makini mradi wa kuku. Siku moja Kudra alipompigia mamake simu, alimskia akilia. Akaamua moyoni mwake kwamba licha ya shida nyingi alizopata Dubai hangemweleza mamake ili asimvunje Zaidi (uk 106). Mawazo yake yalizidi aliposikia mamake alikuwa mgonjwa taabani. Alijiuliza, `je, huko nyumbani anasaidiwa na nani?'

Mtunzi amefaulu kuwasawiri vijana wanaodhihirika kama watu ambao ni tegemeo la wazazi au wazee wao. Katika kubainisha nafasi hii, mwandishi huyu amewatumia wahusika wawili ambao ni Rukia na Kudra.

Riziki ambaye ni mamake Rukia alihamia mtaa ulioitwa Armstadam. Huko alipanga nyumba aliyoilipia shilingi elfu thelathini kwa mwezi. Badiliko hili la hali yake ya maisha lilitokea mara tu baada ya Rukia binti yake kwenda Dubai na kuanza kazi. Alimtilia mamake kila aina ya starehe kama vile kumnunulia friji la milango miwili na redio kubwa ya kumwongoa kwa muziki akitaka. Alimnunulia pia kabati la kuagiza kutoka Malaysia na makochi ya bei.

Kudra alipokumbuka kuwa mamake alimtegemea yeye, alikwenda kwa wakala wa ajira za Dubai mara moja. Alimweleza kuwa mzee wake (yaani mamake) hakuweza kujimudu na alimtegemea yeye kwa kila kitu; chakula, dawa na kodi ya nyumba (uk.63). Kwa jumla vijana katika jamii wanaelewa na kufahamikiwa kuwa wao ndio wanaotegemewa na wazazi wao katika huo uzee kwa kila namna. Vijana wanafanya wanaloliweza ili kuwakimu wazee wao. Bila ya vijana kuweko, wazazi au wazee wao wanajipata katika maisha ya kuteseka kwa kuwakosa watu wa karibu wanaoweza kuwasaidia. Maswala mengi yanawakera vijana hasa wawaonapo wazazi wao swazazi wao wakijitahidi kuwalea na kuwasumbukia licha ya wao kukosa nguvu za kiuchumi. Imani yao kubwa kwa wazee wao inachochewa na hali kwamba umaskini na uchochole unaowakumba wote kama wanajamii unasababishwa na ubinafsi uliomo, ufisadi, unafiki na kutoajibika kwa walio katika mamlaka juu ya watu wao.

### 3. 2. 5 Vijana kama mihimili ya taifa

Mwandishi wa riwaya ya *Pendo la Karaha* anatudhihirishia kuwa jamii ya siku zijazo inategemea vijana ambao ndio msingi wake. Endapo basi msingi huo ni dhaifu na unakosa kudhibitiwa, basi taifa nalo linakosa matumaini. Baada ya uhuru kupatikana viongozi walioshika hatamu walijaribu kubuni sera kabambe kuweza kushughulikia hususan maisha ya vijana. Kwa mfano kulibuniwa Huduma ya vijana kwa Taifa – NYS ili kuweza kuwasaidia vijana wetu wanaomaliza kidato cha nne kupata mafunzo katika taaluma za kazi mbalimbali zikiwemo uwashi, useremala, udereva na umekanika kati ya mengine mengi. Kulianzishwa vilevile na shule za

kuwashughulikia vijana werevu wahitaji kama vile shule ya Starehe Boys Centre ambayo mwanzo iliwashughulikia hususan vijana wa kiume hadi hivi karibuni ilipoanzisha shule ya wasichana. Ingawa juhudi zilikuwepo lakini hazikutatua matatizo ya vijana kikamilifu. Hata waandishi wa kifasihi katika maandishi yao ya hapo nyuma hawakuwachukulia vijana kwa dhati sana katika uandishi huo ambapo majukumu yao ya uhusika hayakuwa muhimu sana. Nchini Kenya, waandishi wasomi wengi wao wakiwa wahadhiri katika vyuo vyetu ndio wamechukua jukumu la kuangazia maswala ya vijana. Haya yamedhihirika katika riwaya kama vile *Nguvu ya Sala (*Wamitila 1999*)* na *Tumaini* (Momanyi 2006), tamthilia kama vile *Maua Kwenye Jua la Asubuhi (*Kithaka wa Mberia) na *Pango* (Wamitila).

Tunapata maelezo kuwa palikuwa na kambi ya washauri wa shirika la kiserikali la NOOMA lililohusika na maswala ya vijana kama vile ya kazi, elimu, mapenzi na mihadarati. Lilithamini vijana kwani ndio mhimili wa taifa nzima. Msanii anasema iwapo vijana wangeshugulikiwa, basi ingekuwa kazi bure. Taifa haliwezi kwenda mbele (uk 136). Msanii anaendelea kusema kuwa shirika hilo lilifanya kazi bega kwa bega na wizara ya vijana ili kujaribu kuinua hali yao. Hata lilitoa mikopo ya kibiashara kwa vikundi vya vijana kuwawezesha kuanzisha biashara. Kwa kuwa shirika hili lilifahamu umuhimu wa vijana katika jamii, mwandishi anasema hii haikuwa mara ya kwanza kwa kundi hilo kufika pwani. Ilikuwa mara ya nne. Mara ya kwanza, ilikuwa sehemu ya Tudor. Mara ya pili, Lilikuwa sehemu ya Kilifi. Mara ya tatu, lilikuwa Malindi mjini na kwamba sasa lilikuwa Mombasa sehemu ya Likoni.

Msanii amemtumia mhusika Kassim ambaye alikuwa amezama katika madawa ya kulevya. Kassim alikuwa amewekwa rumenya na ajuza waliyelewa pamoja na kuishi pamoja kule Bombolulu. Ilimchukua Rehema mamake kumtia Kassim katika kituo cha kurekebisha tabia ndipo akajinasua kutokana na ulevi wa dawa. Rehema, mamake Kassim alikuwa bwanyenye na tajiri mkubwa hapo Mombasa. Alifanya kila jitihada ili kumbadilisha mwanawe aje amfae kama mrithi wa mali yake. Alielewa fika kuwa kijana huyu ndiye ambaye angekuwa ni macho yake kwa kuwa sasa hata uzee ulimfikia (uk 137-138).

Kwa jumla msanii anatumia shirika la NOOMA pamoja na mhusika Kassim kutudhihirishia kwamba vijana ndio nguzo ya taifa na wao ni viongozi wa sasa na

hata baadaye. Ni dhihirisho la juhudi za Taifa kuwapatia vijana maelekezo ya kuwafaa kwa sababu taifa lisilo na vijana ni mfano wa gari bila mtambo au jahazi bila tanga. Ili taifa liwe bora la kutumainiwa, sharti vijana wake walelewe vyema, waelekezwe vizuri, wafunzwe adabu, nidhamu na maadili murua ili waje wawe waaminifu.

### 3. 3 Nafasi hasi wanazopewa Vijana

Mwandishi amefaulu kubainisha nafasi hasi, dhalilishi na za kudunisha ambazo vijana wanajikuta kwazo katika jamii. Jamii ya aina hii ina mfumo unaomwona kijana kama mtu mnyonge na dhaifu na hususan katika masuala ya malezi, uchumi na mapenzi.

#### 3. 3. 1 Uhusiano wa vijana na wazazi wao

Vijana wamechorwa kama watu wasiowatii na kuwasikiliza wazazi wao. Wanafanya hivi kwa kujiona kuwa ni wakubwa na wanaoweza kujiamulia mambo yao wenyewe bila ya kuwahusisha wazazi wao. Jinsi maendeleo ya Rukia kule Dubai yalivyoendelea kuingia masikioni mwake, ndivyo Kudra alivyozidi kutamani kuabiri ndege naye aende Uarabuni. Alimwambia mamake kuwa alitaka kuacha shule lakini mama yake hakutaka kusikia hayo. Kudra hakusikia mawaidha ya mamake hata kidogo kama anavyosema mwandishi:

> Riziki alimweleza binti yake kuwa wapo
> Wasichana waliotaabika katika miji kama
> vile Jeddah, Dubai New York, Berlin na
> Cairo. Hili halikumpigisha mshipa Kudra
> (uk 19-20).

Riziki vilevile alimwambia Kidawa kuwa yeye mwenyewe alikuwa amemkataza bintiye kuhusu kwenda Uarabuni lakini hakumsikiliza hata kidogo. Alimsisitizia kuwa vijana hawasikilizi. Akampa mfano wa Regina aliyekwenda Ujerumani na Mjerumani Vorster aliyemwoza kwa mwanamume mwingine (uk 122).

Baadhi ya matatizo yanayoikabili jamii yanachangia suala la vijana kuonekana kama watu wasiowatii wazazi wao. Baadhi ya mienendo wanayochukua vijana inatokana na msukumo wa hali ilivyo katika jamii yetu kama vile umaskini, mazingira mabaya ya kuishi, kutowajibika kwa viongozi, utoaji rushwa na ukandamizaji unaofanywa na wenye nguvu dhidi ya wanyonge. Kila tukio katika jamii halitokei tu vivi hivi bila

chanzo chake. Kila tukio huwa limeanzishwa na jambo fulani (Ram Roy Bhaskar 1998).

### 3. 3. 2 Vijana na ukosefu wa maadili.

Mhakiki Nyamemba (2013) katika Uchanganuzi linganishi wa maswala ya vijana na jinsi yanavyoshughulikiwa na waandishi katika diwani ya *Tunu ya Ushairi,* alisema kuwa utovu wa maadili umechangiwa pakubwa na maendeleo ya teknologia na wazazi kukosa muda mwingi wa kuwa na watoto wao. Tunaunga kauli hiyo mkono kwani hapo awali, vijana walifunzwa mienendo bora kule jandoni na unyagoni, maana sherehe kama hii ilikuwa ni ya jamii. Zamani kila mtoto alikuwa ni mali ya jamii na watoto walikuwa wakimheshimu kila mmoja kama mzazi wake. Siku hizi mambo ni tofauti kwa kuwa kila mzazi ana jukumu la kumlea mtoto wake mwenyewe, wakati ambapo amefungwa na kazi mbalimbali.

Katika utamaduni wa Kiafrika vijana wa kike hawakuruhusiwa kustarehe na wazee hasa wakati wazee walipokuwa katika sherehe zao. Mwandishi anatueleza kuwa siku moja Lindo aliingia kwa fundi Mwamba, fundi wa baiskeli mwendo wa saa kumi hivi. Hapo kwenye karakana, wazee walizoea kukutana katika mapumziko yao na kucheza bao. Kassim alikuwa akicheza bao na mzee Mwamba ambapo Lindo naye alingojea zamu yake ifike ili atakayeshindwa na mwenzake auondokee mchezo apate kuucheza vilevile. Baada ya muda mfupi, Kassim alishindwa na Mzee Mwamba akatoka na sasa ikawa ni zamu ya Lindo. Mwamba alimwambia Lindo, `unipeleke polepole mwanangu. Mimi ni babako' (uk 46). Masimulizi haya ya msanii yanatupa picha ya jinsi vijana walikosa adabu hata kufikia kiwango cha kuketi na wazee rika za baba zao na kucheza bao pamoja. Mzee Mwamba mwenyewe anakiri kuwa yeye ni sawa tu na babake Lindo.

Suala la vijana kuwekwa rumenya na watu wanaowazidi umri ni suala ambalo hatuwezi kulifumbia macho. Leo kijana msichana atawekwa rumenya na babu mzee. Vilevile kijana wa kiume atawekwa rumenya na nyanya au bibi mzee. Rehema alimtafuta mwanawe Kassim kwa vyovyote vile amsaidie katika usimamizi wa kampuni yake. Alianza kumtafuta kila mahali ikiwemo Maweni, Kongowea, Kisauni na Bombolulu. Mwandishi anatueleza kwamba baada ya miezi minne ya kumsaka, Rehema alielezwa kuwa Kassim alikaa Bombolulu na ajuza wa miaka sitini (uk 77) .

Bi Kidawa naye anamweleza mwenzake Riziki kuwa palitokea visanga hapo kwao Likoni. Kwamba wasichana na wavulana walifumaniwa wakipigwa picha wakiwa uchi na wazungu. Riziki alishangaa na kusema`mambo tunayoyafanya kwa ajili ya pesa hayaaminiki ` (uk 143). Baadhi ya vitendo visivyostahili vinavyofanywa na vijana wetu vinatokea kwa sababu ya uhitaji walionao. Kama ilivyo kwa watu wote kwamba mtu lazima ale, anywe, avae na astarehe ndivyo vivyo hivyo kwa vijana wetu. Kwa kukosa ajira inayoweza kuwakidhia mahitaji kama hayo, baadhi yao inawabidi kujiingiza katika vitendo vya aibu na vinavyoatua moyo. Ndiyo sababu akasesema alivyosema mwana Uhalisia Hakiki Bkaskar (1998) kwamba matukio yanayotendeka katika jamii huwa na visababishi vyake.

### 3. 3. 3 Vijana na kisasi kazini

Msanii amefaulu sana katika kuwasawiri vijana kama watu ambao wanakosa kutilia maanani maadili ya kazi kwa kujilipizia kisasi hasa wanapopata mateso na aina zozote za dhuluma. Kudra alikumbuka mateso na dhuluma aliyokuwa akitendewa na mwajiri wake Aminii na mkewe Nayrat kule Dubai. Alikumbuka kuwa alinyimwa simu ampigie mamake. Akakumbuka hakuruhusiwa kuzungumza na yeyote pale. Akakumbuka chakula cha makombo alichokula baada ya kila mtu pale kula. Akakumbuka kuwa hata mshahara wake alipewa nusu. Mwisho alipokumbuka waajiri wake walimtisha kuwa akijaribu kutoroka watamlimbikizia makosa ili aozee katika jela huko Dubai, mwandishi anatufahamisha alipanga sasa kuwaibia dhahabu na mikufu yao aufidie huo utumwa:

> Sasa ukawa moyo unamshauri akipata hiyo
> dhahabu na mikufu ya matajiri wake ataichukua,
> aifiche ili aufidie huo utumwa wake. Alitafuta
> ufundi wa kuwaibia na kisha kutoroka maana
> pia wao walimwibia, walimnyanyasa. Kwa nini
> wao wamwibie na yeye asiwaibie (uk 106).

> Alimchukulia mwenyeji wake darhim zipatazo elfu
> mia mbili kutoka kwa kasha lake na akateremka
> ngazi, Huyooo! Aliingia treni huku amevalia buibui
> na kikapu cha mwajiri wake na miwani ya jua *(uk 108).*

Teresa Almasi alikuwa kijana msichana aliyefanya kazi kwa Abdulla, jirani yake Aminii aliyekuwa amemwandika Kudra. Teresa alitoka pwani ya Kenya sehemu ya Digo. Walikutana na Kudra akamwambia kuwa yeye hata shilingi moja hakupewa.

Kisa na sababu yake ni kuwa walimkata pesa ya nauli ya ndege na ajenti Rehema aliyampeleka Dubai. Almasi alimwambia Kudra kuwa yeye angepata mali yao, angeichota na akimbie (uk 113).

Kudra aliachishwa kazi na Salim mwajiri wake wa pili baada ya kumfanyia kazi na akatumiwa vibaya kimapenzi. Baada ya Kudra kuzozana na bintiye mwajiri wake na kisa hicho kunaswa na kamera za C.C.T.V za pale nyumbani, Salim alimfukuza na akamnyima mshahara wake wa mwezi huo. Yeye pia alifikiria angalau kumwibia Salim kitu ili iwe ni fidia ya mshahara wake wa mwezi ule lakini akakumbuka onyo la Salim akimshauri aondoke salama na asifanye jambo la ujinga litakalomtia katika matatizo (uk 146).

### 3. 3. 4 Vijana na dhuluma

Vijana wetu katika jamii wawe ni wa kike au wa kiume wanapitia katika aina mbalimbali za dhuluma maishani mwao. Mfano wa dhuluma hizi ni kama vile dhuluma za kikazi na dhuluma za kimapenzi. Katika maeneo yao ya kazi wanadhulumiwa kwa mishahara au ujira mdogo usiowafaa kitu. Wale wa kike na kiume vilevile wanadhulumiwa kimapenzi na waajiri wao.

#### 3. 3. 4. 1 Dhuluma za kikazi

Msanii amewasawiri vijana kama watu wanaodhulumiwa na jamii kikazi. Mfano anaoutoa ni kwa kupitia wasichana waliomfanyia kazi Fauziya katika biashara yake ya ukandaji viungo vya miili pale *Massage Parlour*. Kudra aliahidiwa na Fauziya kuwa kando na mshahara ambao angepata pale, angejipatia pia pesa za ziada endapo wateja wangependa muda zaidi na wa ziada. Mwandishi anasema kuwa hizo pesa za ziada hata zilipotelewa na wale wateja, aliyezichukuwa ni Saumu aliyewasimamia mahali hapo (uk 168).

Aminii na Nayrat walimdhulumu mfanyakazi wao Kudra kwa kumnyima uhuru wake wa kukutana na binadamu wengine hapo kwao nyumbani ila kwa ruhusa yao tu. Walimwachilia ale baada ya kila mtu kula na hakuruhusiwa kula chakula walichokula wao ila makombo. Mwandishi anasema waajiri hawa walikataa kumpa simu aseme na mama hali wakijua kuwa mamake alikuwa mgonjwa.

Mbele ya waajiri wao, vijana wanaonekana kama watu wanyonge na hatima ya maisha yao imo katika mikono ya waajiri. Hawatambuliwi kama watu wenye haki zao japo wao ni wahitaji. Uonevu wanaoonyeshwa ni kutokana na sababu kuwa wao ni watu wanaoonekana kama wanyonge katika jamii. Waajiri wanatumia nafasi ya changamoto zao kama vile uhitaji au umaskini mkubwa walionao kwenye jamii na kuwatumia wapendavyo kwa kuwa hawana kwingine kwa kwenda au kukimbilia na kisha kujinufaisha wao kwa nguvu na jasho lao.

### 3. 3. 4. 2 Dhuluma za mapenzi

Kipyegon (2013) alimnukuu Millet (1969:20) ambaye katika harakati zake za kupinga nafasi chukivu ya mwanamke, anadhihirisha namna mwanaume anavyolishugulikia tendo la ngono kama ishara ya udhabiti na uwezo juu ya wengine (wanawake). Anaangazia kazi ya Jean Genet, The Thiefs Journal, na anafafanua mtazamo wa mwandishi aliyemwumba mhusika Armand. Mhusika Armand anajivunia na kuonea fahari ushindi wake. Armand ananasibisha kitendo cha ngono na udhabiti, uwezo wake na ushindi.

Katika *Pendo la Karaha*, msanii ametusawiria hali sawa na hiyo katika jamii anayotungia kazi yake. Wanaume wawili wanamdhlumu Kudra, kijana msichana na mwajiriwa wao katika nyakati tofauti (uk 107). Mwandishi anasema kuwa Kudra alipomkatalia Aminii huo utashi wake, alianza kumchukia hata zaidi. Kila siku akamtafutia sababu ya kumtukana Kudra (uk 111).

Vijana wanakumbana na dhuluma za mapenzi kila uchao katika maeneo yao mbalimbali ya kazi. Hali hii inatokana na utovu wa nidhamu, tamaa na hali ya kutowajibika kwa matajiri wanaotoa ajira hizo kwa vijana. Aidha wanatumia nguvu zao za kiuchumi na uwezo mkubwa wa mali zao na kuwashawishi vijana hasa wa kike kukubali kuingia katika utumwa wa kutumiwa vibaya kimapenzi. Wengi wanaridhia hali hii kwa sababu ya pesa na mali kidogo wanazopata kutoka kwa waajiri wao ili kujikidhia mahitaji yao wenyewe na ya familia zao maskini.

Alipaojiriwa kazi ya ukandaji miili katika jumba la Massage Parlour, Saumu alimtoa kwa wanaume waliokuja pale kufuatia huduma za kukandwa. Mwandishi anasema,

`Saumu alimlazimisha kwenda na mwanaume aliyeitwa Ali nyumbani kwake. Ali naye baadaye akampeana kwa mwanaume mwingine (uk 170).

Kassim naye alihama na akawekwa rumenya na mwanamke ajuza wa miaka sitini. Mwandishi anatueleza kuwa baada ya miezi minne ya kumsaka, Rehema alielezwa kuwa Kassim alikaa Bombolulu na ajuza wa miaka sitini (uk 77). Rehema mamake Kassim alipobisha hapo kwa ajuza huyu, alimwambia waziwazi kuwa Kassim alikuwa ni wake na wala hangempata. Alisema katika ulevi wake, `Kassim hamumutoboi! Ni waangu, yaani miimi. Ziinduna unaelewa? Eeeh? Eeeh wangu mimi' (uk 79).

Matukio haya yanadhihirisha kuwa vijana ni watu wanaopitia dhuluma za mapenzi katika jamii yetu. Vijana wa kike wanaotumiwa kama wahudumu wa nyumbani wanapitia madhila ya kulazimishwa mapenzi na hao waliowaajiri. Nao vijana wa kiume wanatumiwa kwa kuwekwa rumenya na mabibi waliowazidi umri ili kuwatimizia uchu wao wa mapenzi kwa malipo.

### 3. 3. 5 Ushindani na Ushawishi wa vijana

Vijana wamesawiriwa kama watu wanaoshawishiana na kushawishika kwa urahisi. Wanakosa kudadisi na kutathmini mambo kabla ya kuchukua hatua. Mwandishi anadhihirisha namna ambavyo vijana wanaweza kushawishika kwa haraka. Kudra anashawishika baada ya kushuhudia namna Rukia alivyoyabadilisha maisha ya mamake baada ya kwenda Uarabuni. Kudra alisikia kuwa ile nyumba ambayo Rukia alimpangia mamake alikwishainunua tayari. Pia alisikia fununu kuwa Rukia alikuwa na mpango wa kununua gari na kuwa alikuwa na dola nyingi katika benki. Alisikia vilevile kuwa Rukia alimwajiri yaya kumsaidia mamake hapo nyumbani. Mwandishi anasema: familia ya Rukia iliendelea kuwa kichocheo katika moyo wake. Kudra alijua familia hiyo haikuwa kitu jana lakini leo wanajiweza, kisa na maana ni hiyo kazi ya Dubai (uk 21). Ushawishi huu ulimfanya Kudra amkabili mamake kwa kumpasha habari ya yote aliyoyatenda Rukia. Msanii anasema kuwa licha ya pingamizi za mamake, Kudra aliendelea kumkera (uk 22). Hata hivyo mamake alimwambia, kufanya jambo ni muhimu lakini wakati ukifika. Si vizuri kufanya pupa mwanangu wajua (uk.22).

Hali ya umaskini na uchochole unaoikabili jamii ya mwandishi, inawafanya vijana wengi kushawishiana na kuingia katika maovu ya aina mbalimbali. Baadhi yao wanashawishika na kuingia katika biashara na utumiaji wa dawa za kulevya. Mbali na umaskini, tatizo hili linaweza kuchangiwa na ukosefu wa mikakati thabiti ya maisha adilifu katika familia kwenye jamii.

Mwandishi anasema kuwa vijana wengi waliingia katika utumiaji wa mihadarati bila ya wao kutaka. Walishawishiwa na kudanganywa kuwa wangenufaika kwa kutoka katika umaskini wao. Mwandishi anasema, wengine waliingia sio kwa kutaka. Waliingia kwa kuwa waliahidiwa utajiri; magari, nyumba, ploti za ufuoni na vitu vingine vya starehe. Haikuwa nia ya vijana wengi. Hata hivyo waliingia tu wasijue wanaingia katika utumwa na mtego ambao si rahisi kutoka mradi umetia guu lako (uk.31).

Vijana katika jamii wanashawishika hasa baada ya kushuhudia jinsi wenzao waliosafiri Uarabuni wanavyowainuwa wazazi wao kiuchumi. Wanawajengea majumba na kuwanunulia magari. Hivyo basi wanatamani kuwa kama wenzao. Wengine wengi wanakuwa waraibu wa mihadarati kwa kudanganyika kuwa usambazaji wa dawa hizi za kulevya ungewapa mishahara minono. Mwisho wakajipata katika mtego ambao ni vigumu kujinasua.

### 3. 4 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia nafasi wanazochukuwa vijana katika jamii. Imejitokeza kwamba vijana wanachukuwa nafasi chanya pamoja na nafasi hasi.

Baadhi ya nafasi chanya zilizojitokeza ni pamoja na kwamba vijana ni wenye uhuru wa mawazo kwa kujikomboa kimawazo, wenye maadili kwa kuwa na misimamo imara dhidi ya vishawishi vinavyoweza kuwaingiza katika maovu ya uasherati, wenye ari ya kujikomboa kiuchumi, wenye majukumu ya kuwatunza wazazi pamoja na kuwa ni mihimili ya taifa.

Nafasi hasi kwa vijana zimejitokeza kwa sababu ya kuwepo kwa jamii inayomwona kijana kama mtu mnyonge na dhaifu hasa katika masuala ya malezi, uchumi na mapenzi. Kwa mfano, anakosa maadili kazini, wenye kisasi kwa waliowaajiri, ni

washindani na wenye wingi wa ushawishi na kushawishiana kwa urahisi na hivyo kukosa makini katika kudadisi mambo kabla ya kuchukuwa hatua juu ya yale yanayowahusu.

## SURA YA NNE

## TATHMINI YA HALI YA JAMII KATIKA *KOVU MOYONI*

### 4. 1 Umaskini katika riwaya ya Kovu *Moyoni*

Umaskini ni tatizo linalokumba jamii ya riwaya ya *Kovu Moyoni.* Emoro alitoroka kwao na kwenda kutafuta ajira kutokana na umaskini uliowakumba baada ya babake kuoa wanawake watano akawa hajabahatika kupata chochote kwa baba yake. Baada ya mapigano ya kikabila kumpata Muhoroni na Lome, alikimbilia Rama. Hapo alinunua robo ekari ya shamba na akajenga kibanda cha nyasi. Chumba cha kulala alikitumia pia kama chumba cha kupikia chakula vilevile. Sehemu ya sebule aliitumia kama stoo ya majembe na karai mbovu za kuogea. Hakuwa na meza ila stuli moja kuukuu aliyoitumia kama meza. Alipoulizwa na Boke sababu za yeye kutooa, alisema kuwa yeye hakuwa na pesa za kumpa bibi akisema suala hilo liachiwe wenye uwezo (uk 3-5).

Jamii ya Mzee Makoti ilinyang'anywa shamba lao na likapewa bwanyenye mmoja kutoka Dunga. Hapo ndipo Meja-K na mamake walipofanya kazi kama vibarua na wakalipwa pesa na posho kidogo. Familia hii ikabakia katika umaskini mkubwa kwa sababu sehemu ndogo walioachiwa haikuweza kuikidhia familia yao ya watoto saba (uk 15) .

### 4. 2 Ubwanyenye katika *Kovu Moyoni*

Jamii ya Kovu Moyoni imejengwa vilevile na matajiri wanaomiliki mashamba na mali nyingi kupindukia. Baadhi yao wamejipatia mali hiyo kwa kuwanyang'anya wasio na nguvu. Bwanyenye mmoja kutoka Dunga alinunua shamba kubwa ambamo alipanda pamba. Aliajiri vibarua humo waliofanya kazi na akawapa mshahara wao mdogo (uk 16). Bosi ni mhusika tajiri aliyemiliki shamba kubwa kuliko yote. Msanii anasema kuwa huyu alikuwa ni mtu maarufu katika serikali na pia alikuwa ni mtu mwenye asili na fasili. Baba yake Bosi alikuwa pia ni bwanyenye mtajika. Katika shamba hili alifuga wanayama kama vile twiga, simba, chui, duma, sungura, kima, nyani na wanyama wengineo (uk 50) .

Korir alikuwa ni mbunge bwanyenye ambaye alijilimbikizia mali nyingi katika mabenki. Alitegemewa na watu wengi katika kuwakidhia mahitaji yao. Yeye

mwenyewe alikuwa na wanawake takriban saba na watoto waliomtegemea thelathini (uk 75).

Kwa jumla hii ni jamii yenye watu wenye ubinafsi mkubwa. Wenye uwezo wa kiuchumi wanaendelea kuwanyang'anya kidogo walichonacho watu maskini. Viongozi wanajilimbikizia mashamba na misitu ya kufuga wanyama mwitu wakati jamii inakosa mashamba ya kulima. Pesa nyingi katika mabenki na mashamba makubwa yanawafanya hata kuoa wanawake wengi.

### 4. 3 Vijana na madawa ya kulevya

Mwandishi wa riwaya ya *Kovu Moyoni* amedhihirisha kuwa jamii anayoandikia ni jamii inayoshuhudia usambazaji na matumizi ya madawa ya kulevya miongoni mwa vijana wake. Hili ni jambo la kusikitisha tunapoona jinsi vijana wanavyojitumbukiza katika janga la kutumia, kusafirisha na kuuza mihadarati kwani vijana ndio nguzo na matarajio ya taifa lolote.

Vijana kama vile Yoko alipotoroka mashambulizi ya kikabila kwao Rama, alikimbilia mji wa Dunga. Alikosa usaidizi wowote wala kazi ya kufanya. Baada ya kuzunguka katika kila mtaa wa Parklands kwa vibariwa ambavyo havikupatikana kila mara, tatizo hilo lilimfanya aingie katika mtandao wa dawa za kulevya. Shughuli yake mpya ilimpeleka ng'ambo hadi Paris na New York. Yoko akawa akizunguka hivyo kusambaza dawa, kuchukuwa ripoti na hata kuwahonga polisi.

Vita vya kikabila vinavyotokea katika jamii ndivyo vinavyosababisha baadhi ya jamii kuzihama sehemu zao za makazi walizozoea. Katika maeneo kama hayo, kila mtu katika jamii huwa amekita mizizi yake hapo na huwa na shughuli mbalimbali zinazohusu kujiinua kiuchumi. Wengine wanapokuwa ni wafugaji, wengine huwa ni wakulima na wengine wafanyabiashara. Mashambulizi ya kikabila yanapotokea, jamii hutawanyika na kuzitupilia mbali shughuli zao. Tatizo hili huwatia watu katika dhiki ya kukosa ajira na hali ya maisha huwa ni ya chini sana.

Kiunzi mojawapo cha nadharia ya Uhalisa Hakiki kinatutaka tusawiri matukio kihistoria pale ambapo wahusika wanatekeleza matendo yao kitabaka aidha kimakusudi au bila kufahamu. Tabaka la viongozi hulaumiwa mara nyingi pamoja na

kushukiwa kwa kutowajibika ipasavyo juu ya suala la mapigano yanayowaacha vijana bila kazi baada ya kufurushwa na kuwaacha bila linguine la kufanya ila biashara haramu ya madawa na maovu mengine. Lawama huwa kwamba tabaka ambalo huonekana limeongoza jamii kwa muda mrefu hupata wapinzani baadaye ambao nguvu zao huwa ni kupitia kuchochea jamii dhidi ya jamii nyingine kwa lengo la kuwafurusha kwao endapohawaonekani kuunga mkono kundi linalotaka kuchukua uongozi. Hivyo basin i kupitia matukio kama hayo ya kihistoria ambapo vijana hujikuta katka biashara inayoharamishwa ya ulanguzi wa mihadarati.

### 4. 4 Dhuluma na unafiki wa viongozi walio mamlakani

Mwandishi wa riwaya ya *Kovu Moyoni* amedhihirisha kuwa jamii anayoandikia ni jamii inayoshuhudia usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana wake. Hili ni jambo la kusikitisha tunapoona jinsi vijana wanavyojitumbukiza katika janga la kutumia, kusafirisha na kuuza mihadarati kwani vijana ndio nguzo na matarajio ya taifa lolote.

Vijana kama vile Yoko alipotoroka mashambulizi ya kikabila kwao Rama, alikimbilia mji wa Dunga. Alikosa usaidizi wowote wala kazi ya kufanya. Baada ya kuzunguka katika kila mtaa wa Parklands kwa vibarua ambavyo havikupatikana kila mara, tatizo hilo lilimfanya aingie katika mtandao wa dawa za kulevya. Shughuli yake mpya ilimpeleka ng`ambo hadi Paris na New York. Yoko akawa akizunguka hivyo kusambaza dawa, kuchukua ripoti na hata kuwahonga polisi (uk 73).

Vita vya kikabila vinavyotokea katika jamii ndivyo vinavyosababisha baadhi ya jamii kuzihama sehemu zao za makazi walizozoea. Katika maeneo kama hayo, kila mtu katika jamii huwa amekita mizizi yake hapo na huwa na shughuli mbalimbali zinazohusu kujiinua kiuchumi. Wengine wanapokuwa ni wafugaji, wengine huwa ni wakulima na wengine wafanyabiashara. Mashambulizi ya kikabila yanapotokea, jamii hutawanyika na kuzitupilia mbali shughuli zao. Tatizo hili huwatia watu katika dhiki ya kukosa ajira na hali ya maisha kuwa ya chini sana.

Kiunzi mojawapo cha nadharia ya Uhalisia Hakiki kinatutaka tusawiri matukio kihistoria pale ambapo wahusika wanatekeleza matendo yao kitabaka aidha kimakusudi au bila kufahamu. Tabaka la viongozi hulaumiwa mara nyingi pamoja na

kushukiwa kwa kutowajibika ipasavyo juu ya suala la mapigano yanayowaacha vijana bila kazi baada ya kufurushwa na kuwaacha bila lingine la kufanya ila biashara haramu ya madawa na maovu mengine. Lawama huwa kwamba tabaka ambalo huonekana limeongoza jamii kwa muda mrefu hupata wapinzani baadaye ambao nguvu zao huwa ni kupitia kuchochea jamii dhidi ya jamii nyingine kwa lengo la kuwafurusha kwao endapo hawaonekani kuunga mkono kundi linalotaka kuchukua uongozi. Hivyo basi ni kupitia katika matukio kama hayo ya kihistoria ambapo vijana hujikuta katika biashara inayoharamishwa ya ulanguzi wa mihadarati

Msanii anatusawiria aina za nyumba zilizomilikiwa na mbunge mmoja. Nyumba alimoishi Mali ya Mungu ilijengwa kwa mabati, juu na chini. Ilijengwa karibu na mto na katika eneo lililotupwa takataka za kila aina vikiwemo vigae vya chupa, ngozi, betri, mipira na mabaki ya chakula. Wakiwa ndani waliweza kuwaona ndege kama kunguru, tai, korongo na mwewe wakipigania masalia ya vyakula vilivyotupwa kutoka viwandani Dunga. Baridi kali iliingilia katika fremu za kilango cha bati ambacho mwandishi anasema kililia kila upepo ulipovuma nje. Hata mvua iliponyesha, maji yalipenya ndani ya nyumba hiyo. Kila mwezi mbunge huyu aliongeza kodi yake ya mwezi licha ya uduni na adha za nyumba hizo zilizoenea Kabare, Mlelea na Usatu (uk 69).

Chifu Senge naye alimnyang'anya mkimbizi nyumba yake nzuri ya ghorofa. Kwa kuona kuwa nyumba hiyo iliezekwa kwa vigae vizuri vya kuvutia na sakafuni vigae vya sini, Chifu aliingia humo na akarithi kila kitu. Msanii anasema Chifu alirithi mifugo, samani na vyombo. Alirithi hata shamba kubwa la ngano la huyo mkimbizi ambaye aliruka majini na kujiua kwa kuudhiwa na vitendo vya Chifu huyo (uk 32).

Ishmael aliyekuwa akimuuguza mbunge aliyeitwa Zunga, hakutaka kurudi nyumbani kwao kwa sababu alijua hakuwa na shamba huko. Msimulizi anasema kuwa mbunge na mwanasiasa maarufu kwa jina Mwamba alilichukuwa shamba la babake Ishmael kwa nguvu na kwa vitisho. Mbunge huyo alisababisha babake Ishmael kufungwa jela pasipo sababu kwa kusingiziwa kuwa alikuwa akiuza bangi (uk 76). Unafiki wa viongozi unadhihirika katika jamii ya msanii wa riwaya ya *Kovu Moyoni*. Unafiki ni utovu wa ukweli katika mwenendo wa binadamu hasa kwa lengo la kujipatia sifa. Mnafiki hutenda vema kwa nje, lakini nia yake si kufuata dhamiri yake na maadili

anayojua ni mazuri, bali ni kupendeza watu wengine ili kupata faida fulani kutoka kwao.

Mashambulizi ya mara kwa mara ya kikabila yanayoshuhudiwa katika jamii anayoandikia mwandishi, yanatokea kutokana na unafiki mkubwa kati ya viongozi na wenye mamlaka kama vile machifu. Chifu Senge alikuwa akihimiza amani mchana akiwa katika mabaraza. Usiku ulipofika yeye ndiye aliyeshiriki katika kupanga mashambulizi. Msanii anamwelezea kama kinyonga kwa sababu alibadilika kulingana na wakati na hali. Alifanyia serikali kazi mchana na mwandishi anasema mtu angedhani ni malaika. Usiku Chifu Senge ndiye aliyeshiriki tandabeluwa na ndiye aliyefichua siri za wakazi wa eneo la Siloko (uk 31).

Mwamba alikuwa mbunge mheshimiwa. Alipanga mkutano wa kwanza na vijana saa nne za usiku ili kupanga mikakati ya mashambulizi. Aliposimama kuwazungumzia vijana usiku huo, alisema kuwa walijumuika hapo kuzungumzia masuala ya maendeleo. Alisema kuwa yeye angependa mgombea kiti cha ubunge cha eneo bunge lao awe ni msululu, mtu wa kabila lake. Mkutano huo ulifungwa saa saba za usiku (uk 53).

Utendakazi wa maafisa wa usalama pamoja na mahakama unalaumiwa pakubwa katika jamii ya *Kovu Moyoni*. Vyombo hivi viwili, usalama na mahakama, hutenda kazi zao kwa pamoja. Vyote vinategemeana sana na kimoja hakiwezi kufaulu katika majukumu yake bila kingine. Hii ni kwa sababu vyote hivi huongozwa na sheria ya nchi ambayo imepitishwa na kuwekwa katika muongozo wa katiba ya nchi. Hata hivyo usalama na mahakama vinakosa kuwa makini zinapofanya uchunguzi na hivyo kutoa maamuzi na hukumu zisizostahili na kuiachia jamii makovu yasiyofutika.

Mwita alishikwa na jeshi la vijana akitoroka mapigano yaliyowafurusha wengi kutoka katika mashamba yao. Baada ya miezi mitano, ndipo yeye na wenzake hamsini walifaulu kulitoroka jeshi hilo. Walipofika eneo la Siloko madukani, hapo wakakutana na jeshi la serikali la nchi kavu. Mwita na wenzake walishikwa na jeshi hili la serikali licha ya kuwaelezea kuwa wao hawakuwa wanachama wa jeshi la vijana. Jeshi la serikali lilishikilia kuwa Mwita na wenzake walikuwa ni wanachama wake. Walitiwa katika lori kubwa la jeshi wakapelekwa katika kituo cha polisi

kungojea mashtaka (uk 46). Baadaye Mwita alifikishwa kizimbani na akashtakiwa kwa kuzua rabsha, kushiriki mauaji, ubakaji na hali ya kuvuruga amani ya nchi tukufu ya Tandika. Mwita hakujibu kukubali mashtaka hayo ila alimwambia hakimu alijuwa wazi kwamba Mwita hangeishinda kesi hiyo. Mwita alihukumiwa kifo na akanyongwa. Baadaye kidogo walileta vijana waliokuwa na makosa madogo madogo. Alikuwepo mmoja aliyeitwa Mwita Ngozi.

Hakimu alishangaa kusikia kuwa huyu pia aliitwa Mwita kwa kuwa alidhani ndiye aliyenyongwa. Mwita alimwambia hakimu kuwa huyo Mwita aliyenyongwa alikuwa mateka tu wa jeshi la vijana (uk 135). Tukio hili linadhihirisha kuwa vitendo vya uhalifu havichunguzwi kwa kina. Washukiwa hawachunguzwi na ukweli kupatikana. Vijana wanapata adhabu ambazo hawazistahili katika jamii. Vijana wengi wamewekwa katika korokoro za polisi kwa muda mrefu wakingojea hukumu kwa kushukiwa kutenda uhalifu. Wengine wanatumikia vifungo ambavyo hawakuvistahili.

Viongozi wanasawiriwa kama watu wanafiki na wachochezi katika jamii. Wanawachochea watu wao ili wazue rabsha zinazowatimua watu ambao hawawataki. Watu ambao labda wanaweza kutowarudisha mamlakani. Wanapanga mikutano na kusema ni mikutano ya maendeleo lakini hakuna masuala ya maendeleo yanayoguziwa hapo ila ni uchochezi tu.

Viongozi wanashukiwa kuongoza katika uovu wa dhuluma kwa wanyonge. Wana wanyang`anya watu nyumba walizojenga kwa jasho lao na hata kurithi mali zao. Wanayachukuwa mashamba ya watu wanaowaongoza na ili kuwanyamazisha, wanawasingizia maovu ya uwongo ili wafungwe jela na wao wabaki wakiyatumia na kufurahia jasho la watu wengine.

### 4. 5 Swala la amani na vita

Mashambulizi ya vita vya kikabila katika jamii ya *Kovu Moyoni* ni suala ambalo mwandishi ameliangazia kwa kiasi kikubwa sana. Haya ni mashambulizi ambayo yameonekana kuzuka mara kwa mara na hususan kipindi cha uchaguzi kinapokaribia. Hii ni hali sawa na jinsi mambo yanavyoshuhudiwa katika mataifa mengi ya Afrika ambapo vita vya kikabila huzuka pale uchaguzi unapokaribia. Tatizo hili linapokuja,

serikali hulazimika kuwatuma maafisa wa usalama kukabiliana na wanaozua vurugu hii. Juhudi nyingine inayofanywa na viongozi ili kuleta amani na kukomesha mashambulizi ya mara kwa mara ni kuunda tume za amani na maridhiano ambazo hutembelea maeneo yanayoathirika na kutafuta masuluhisho ya kudumu. Viongozi wa kisiasa katika maeneo yanayokumbwa na vita hivi wamekuwa wakinyoshewa kidole kwa kushukiwa kuchochea vita hivyo.

Jamii ya *Kovu Moyoni* inakumbwa na vita vya mara kwa mara. Mhusika Boke anakumbuka jinsi wageni walivyofukuzwa kama alivyofanyiwa mhusika Emoro kwa kuwa alikuwa mgeni hapo Rama. Alikimbilia maeneo ya Muhoroni na kwa vipesa vyake vichache akanunua kishamba cha robo ekari. Msanii anasema, ` msimu wa kura ulipofika, wanasiasa walianza kugombana kwa ajili ya kura` (uk 4). Machafuko mengine yakazuka na Emoro akatoka hapo Muhoroni kama mtu aliyeoga na nguo zake mkononi. Alikimbilia sehemu ya Lome ambayo nayo pia ilikumbwa na vita vya kikabila. Kutoka Lome, Emoro akatorokea pande za Rama. Rama nako wageni walifukuzwa kama swara. Emoro alikimbia akaingia ndani ya shamba la miwa. Msanii anasema kuwa Emoro alitiwa majani makavu akateketezwa hadi akabakia jivu tu (uk 2) .

Boke na mwanawe Mwita waliona moto mkubwa wakiwa nje ya nyumba yao usiku. Moto huo uliteketeza nyumba huku watu wakiendelea kulia na vilio vikishuka mabondeni kwa huzuni. Walisikia risasi pia zikifyatuliwa mlimani kulipokuwa na mashamba yaliyogombaniwa na makundi yaliyokuwa hasimu. Kuna kundi lililodai ndilo la asili na jingine likidaiwa kutoka nchi jirani. Mwandishi anatueleza kuwa yeyote ambaye hakuwa mwenyeji alitafuta njia yake arejee alikotoka hasa baada ya makaratasi kusambazwa baada ya mkutano wa chifu na mkuu wa wilaya.

Kwa jumla jamii inakumbwa na vita kila uchaguzi unapokaribia. Baadhi ya viongozi wa kisiasa na wa serikali wanashukiwa kuvichochea vita hivyo. Jamii inayodhaniwa kutomwunga mkono kiongozi wa mrengo fulani, ndiyo inayofurushwa ili isishiriki katika kuwachagua viongozi wao. Vita vinaenea katika sehemu kubwa ya nchi na hivyo kuwafanya watu kuwa wakimbizi katika nchi yao.

### 4. 6 Maovu ya ubakaji na unajisi

Haya ni maovu yanayoshuhudiwa kutokea katika jamii ya riwayani. Ubakaji na unajisi unatekelezwa na vijana wanachama wa jeshi la vijana ambalo linafanya mashambulizi yake kwa wageni waliojipatia mashamba katika maeneo yao. Jeshi hili la vijana linawateka vijana wa kiume na wale wa kike waliokataa kujiunga nao. Wanaposhambuliwa, jeshi la vijana linawaelekeza katika kambi zao ambako wanafanyiwa hiana. Wengine wanabakwa wakiwa kwao vijijini wakati jeshi hili linapoingia.

Mfano wa kijana wa kike anayeshikwa na jeshi hili alikuwa ni Eddah bintiye Boke. Alipofaulu kutoroka kutoka katika mikono ya jeshi la vijana, alimwambia mamake kuwa alikuwa ameshikwa na jeshi la vijana waliomdhulumu kimapenzi. Eddah alimwambia mamake, `nilipelekwa msituni. Kazi yangu ikawa ni kuwapikia nikiwafulia huku nikitoa huduma za mapenzi kwa askari' (uk 22-23). Boke vilevile alimkumbuka shangazi yake mwenyewe aliyeitwa Bi. Eddah kama mwanawe. Shamba lake la ngano na mahindi lilipoteketezwa na genge la wapiganaji alifanya ubishi nao. Hii ilitokea miaka kumi hivi iliyopita. Ubishi wake huo ulimpelekea kunajisiwa na vikundi tofauti tofauti (uk 23-24).

Mtunzi anaeleza kuwa tokea alipouawa Chifu Ngata ambaye alipinga vita vya kikabila na hujuma waliyotendewa wanawake, ni kama kiberiti cha mauaji na ubakaji kiliwashwa tena Rama. Watu waliuawa na jinamizi la ubakaji likaendelezwa. Ikawa hata ubakaji ukitokea haikuwa muhimu kuuzungumzia.

### 4. 7 Athari ya ukosefu wa ajira

Idadi kubwa ya wahusika katika riwaya ya *Kovu Moyoni* ni ya vijana wasiokuwa na ajira. Katika jamii hii, wao ndio wanaoathirika kuliko watu wengine wote. Siku moja Mali ya Mungu akizunguka mji wa Dunga aliyaona majengo marefu na akawachukia wale waliokuwa na uwezo mkubwa wa mali kwa kuwa yeye hakuwa nayo. Msanii anasema kuwa Mali ya Mungu alianza kujiona katika kapu moja na wale malofa wa kule kwao Rama. Hao walikuwa ni wale vijana waliokosa la kufanya ambao baadaye waligeuka na kuwa jeshi la vijana (uk 67).

Mtunzi anatusawiria jamii ya vijana iliyokuwa sasa imejaa katika miji kadha. Mchana mzima walionekana wakicheza karata huku wengine wakizunguka na kuwaibia watu wasiotahadhari nao. Miji na masoko yake yakawa lazima mtu ajihadhari sana anapoitembelea wasije wakampiga mtu mwereka na kumchukulia kitu chake. Msanii anasema kuwa walifanya hivyo ili nao wapate kula na kuvaa (uk 71). Katika mji wa Dunga, tunaelezewa kuwa Mali ya Mungu aliendelea kustaajabishwa na visa zaidi vya vijana wa Rama waliozunguka Dunga kwa riziki. Aliweza kuyaona makundi fulani ya vijana yakiwa vibarua na mengine yakizurura ovyo barabarani bila kuwa na mbele wala nyuma.

Suala la ukosefu wa ajira kwa vijana limesawiriwa jinsi lilivyo hata katika jamii katika mataifa mengi. Kulingana na kiunzi mojawapo cha Uhalisia Hakiki ni kwamba uhakiki wa matukio kama haya ya ukosefu wa ajira katika jamii uwe ni wa kufanyika kulingana na uzosefu au tajiriba ya binadamu katika mazingira yake. Hii ni picha halisi ya jinsi hali ilivyo leo katika jamii zetu. Jamii ya vijana inapokosa ajira na kukosa la kufanya, hupata hisia za kuwa na hasira hasa baada ya kushuhudia watu binafsi wanaojilimbikizia mali nyingi. Vijana wanaishia kufanya maovu kama ya wizi wa mabavu na uchopozi kwa wapita njia wasiokuwa na habari.

## 4. 8 Hitimisho

Kutokana na maelekezo ya nadharia yetu ya Uhalisia Hakiki, sura hii imehusika na kuitathmini jamii katika riwaya ya *Kovu Moyoni.* Jukumu hili linatokana na sababu kwamba namna maisha na hali ya jamii ilivyo ndivyo inayowaelekeza vijana katika kuchukua nafasi zao mbalimbali, ziwe ni hasi au chanya.

Kwa jumla sura hii imetutayarisha katika kuziangalia nafasi za vijana katika kazi itakayofuata. Baadhi ya masuala yaliyojitokeza ni usambazaji na matumizi ya madawa ya kulevya miongoni mwa vijana, dhuluma na unafiki wa walio katika mamlaka pamoja na maovu ya ubakaji na unajisi kama namna ya kulipiza kisasi kwa baadhi ya jamii kwenye riwaya inayohusika.

Suala la amani na vita hususan vita vya kikabila limejitokeza kwenye jamii pamoja na athari ya ukosefu wa ajira kwa vijana, hii ikiwa ni picha halisi ya jinsi hali ilivyo leo katika jamii zetu.

# SURA YA TANO

## NAFASI YA VIJANA KATIKA *KOVU MOYONI*

### 5. 1 Utangulizi

Mwandishi wa riwaya hii anaangazia uwezo na mchango muhimu wa vijana katika ujenzi wa jamii. Aidha anadhihirisha uwezo na nguvu walizonazo vijana na ambazo zikiimarishwa zitakuwa msingi muhimu katika jamii yenyewe. Kwa mfano vijana hujiamini kuwa wanaweza kupambana na hali fulani katika jamii. Wao huamua wanayoamua na hawarudi nyuma katika ndoto zao. Hukabiliwa na changamoto zinazoweza kuibuka katika harakati za kujiendeleza aidha kazini au nyumbani. Wao hutumia uwezo, ukakamavu na udhabiti kama mizani ya kujipimia.

### 5. 2 Vijana na ari ya Kujikomboa Kiuchumi

Msanii amewasawiri vijana kama watu wenye ari na bidii ambao wanauelewa mzigo ulio na wazazi wao wajane katika juhudi zao za kuwalea wao na kuwakimu. Katika jamii inayokumbwa na vita vya mara kwa mara vya kikabila, baadhi ya vijana wanachukua jukumu la kuwasaidia wazazi katika kipindi kigumu cha maisha. Eddah bintiye Boke aliona kuwa mzigo wa mamake kama mjane ulikuwa mzito. Hii ndiyo sababu iliyomfanya kujishughulisha katika kazi nyingi bila kuchoka na kuona kuwa zingewaletea pesa angalau kidogo. Mwishowe aliamua kujitosa katika upishi wa maandazi. Hata mamake alimpa heko kwa juhudi zake (uk 42).

Kijana mwingine aliyeitwa Ndori na aliyempa makao ya muda rafikiye Mali ya Mungu, alikuwa na bidii sana kazini mwake alikoajiriwa. Alikuwa anatoka alfajiri sana kwenda kazini. Alikuwa akirudi jioni ila tu pale alipokuwa na kazi nyingine ya ziada ndipo alipoingia usiku (uk 64). Mali ya Mungu naye alitaka kufanya bidii maishani ili apate vile vile kumsaidia mama yake na baba yake katika shughuli zao za kulima na zingine (uk 65).

Vijana wengine ni Abuu, Belinda na Amina. Abuu alikuwa ni mhanga wa vita lakini muuza magazeti maarafu. Belinda na Amina walifanya kazi katika klabu cha Nyota ya Mlimani. Walifanya bidii iliyowavutia wateja wengi hapo kazini. Amina alikuwa shupavu kwani hata alipolewa kidogo tu, alihitaji usingizi kidogo tu na ulevi

ukamtoka akaendelea kuchapa kazi. Msanii anasema 'wateja wengi walipenda walivyoendesha baa ile. Walifanya kazi kwa bidii' (uk 115).

Kijana Emoro alipoona babake amemwoa mke wa tano, akajua kuwa hangebahatika kupata chochote kutoka kwa baba yake. Alitoka nyumbani na akaajiriwa kazi ya kukata miwa kule Muhoroni. Kazi hiyo ilipomshinda akaajiriwa na Mabruk kufanya kazi ya nyumba. Baada ya kifo cha mwajiri wake, alinunua kishamba kidogo hapo. Machafuko ya kisiasa yalipoingia, alikimbilia Lome alikoajiriwa kama mchungaji wa mifugo na Mama Helena. Lome nako kulipoharibika kwa vita vya kikabila, majirani zake wakamtimua hadi Rama. Rama akanunua robo ekari ya shamba. Hapo Rama ndipo mauti yake yalipompata (uk 3-4).

Vijana katika jamii wanatia bidii ili kujaribu kujikimu katika maisha. Bidii na ari yao inatokana na uelewa wao kwamba wamo katika jamii iliyojaa shida za uchochole na maovu mengi ya kijamii yakiwemo kutowajibika kwa serikali na viongozi wa kisiasa kwa sababu ya ubinafsi mkubwa unaowakumba.

### 5. 3 Vijana na uzalendo

Baadhi ya vijana ni waaminifu na wazalendo. Bw. Gondi alikuwa ni mkuu wa wilaya. Msanii anasema kuwa alikuwa bado kijana mdogo. Katika mkutano wa kuleta amani kwa makundi yaliyozozana alikaribishwa na Chifu Senge ili aseme na watu. Mwandishi anasema kuwa Bw. Gondi hakuwa na furaha aliposimama kusema. Alisema kuwa serikali ilipata malalamishi ya uporaji, ubakaji na mauaji ya watu wasio na hatia. Aliwatahadharisha dhidi ya kundi la jeshi la vijana kuwa lilikuwa ni kundi haramu. Halikutambuliwa na kuwa kama serikali ingelipata kundi hilo, ingeliadhibu vikali (uk 20).

Kijana Emoro alipokuwa akiwachunga ng'ombe wa Helena, alipenda kukichukua kiredio chake kidogo. Alikuwa na mazoea ya kuimba nyimbo za kizalendo kila alipozisikia zikiimbwabwa redioni. Hata akiwa bafuni, aliimba nyimbo za kitaifa akisifia watu wake na mashujaa waliojitolea mhanga kupigania uhuru wa nchi yake ya Tandika (uk 4).

Mali ya Mungu aliyeajiriwa katika kampuni ya uuzaji magari, anaelezewa na mwandishi kuwa alipendwa sana kazini. Alikuwa mwepesi wa kutumwa. Alisikiliza akielezwa jambo. Pale kazini walimpenda kwa jinsi alivyokuwa mdamisi na mtu asiyependa matata (uk 64). Vijana wengi ni wazalendo wasiopenda kujiingiza kataka vitendo vinavyokwenda kinyume na sheria na maadili ya kijamii. Mfano ni huyu Mali ya Mungu aliyeapa kwa kukionyesha juu kidole chake cha shahada kuwa yeye licha ya umaskini wake, hangeingia katika shughuli za magawadi kama rafikiye Situma. Akasema hata kama ni kufa, aachwe afe tu (uk 72*)*.

Uzalendo wa vijana unawaongoza katika kusimama kidete dhidi ya vishawishi vya wenzao. Wanasimama imara dhidi ya kujiingiza katika biashara ya mihadarati ili wapate pesa za haraka. Kwa mfano Situma alimpigia simu Mali ya Mungu usiku mmoja naye akakataa kuichukua simu hiyo. Aliitia simu hiyo katika mfumo wa *silent* na kuipuuza. Akaapa ikikatika tu angeizima. Mali ya Mungu alijiuliza ni mara ngapi ashamwambia hawezi kuingia kwenye mtandao wao wa kuzungusha dawa lakini naye haelewi? (uk 77).

Vijana wanaposingiziwa vitendo ambavyo hawakuvitenda, hawatikisiki kwani wanaongozwa na huo uzalendo. Baadhi yao wako radhi hata kufanya lolote katika juhudi za kuisimamia haki yao. Mfano ni Mwita aliyeshukiwa kuwa ni mwanachama wa jeshi la vijana. Yeye alikataa katakata kujibu maswali aliyoulizwa na hakimu. Alimwambia hakimu waziwazi kuwa amfunge tu kwa sababu hata yeye mwenyewe hakimu, alijua kwamba hangeishinda kesi hiyo. Kabla ya kunyongwa, Mwita alimwandikia mamake barua. Sehemu moja ya barua hiyo ilisema, `nina furaha kwenda kuishi katika ulimwengu wa pili nikitumai huko nitapata kupumzika na kwamba kuna haki, salama, ukweli na usawa. Mimi kipenzi chako Edwin Mwita' (uk 132).

Vijana wana misimamo imara ya kizalendo. Wanaipenda nchi yao na wanatosheka popote pale walipo mradi wayapate masilahi yao. Hawataki kuyumbishwa hapa na pale. Wanapolishika jambo, wanakosa imani juu ya kwingineko au mambo mengine. Changamoto zinazowakabili haziwaruhusu kuyumba kutoka sehemu moja hadi nyingine au kutoka kwa wazo moja hadi kwa wazo jingine.

### 5. 4 Nafasi hasi wanazopewa Vijana

Mwandishi amedhihirisha na kubainisha nafasi za kudhalilisha wanamowekwa vijana katika jamii. Jamii ya aina hii huwaona vijana kama watu dhaifu na wanyonge na wenye kuwategemea wenye uwezo wa kiuchumi. Huwaona vijana kama watu wasioweza kujifanyia lolote la maana kwenye jamii

#### 5. 4. 1 Vijana na Maovu

Ukosefu wa maadili ni suala linaloikumba jamii ya vijana katika ulimwengu. Kunao wataalamu wa maswala ya vijana na elimu ambao hudai kuwa elimu bora humfanya mtu kuwa na utu. Kwamba kukosa elimu katika karne hii humtia binadamu katika mikururo ya mikasa (Murono 2005).

Jioni moja Eddah akiyatayarisha maandazi, mlango wao ulivunjwa. Kundi la watu kumi na wawili liliingia ndani likiwa limejihami kwa bunduki na mishale. Liliomba pesa na hatimaye likaishia kumnajisi Boke na bintiye Eddah. Boke alinajisiwa akabaki hali hoi. Hili lilikuwa ni jeshi la vijana lililomfanya Eddah kila asikiapo sauti nje akaona ni kama wanarudi tena (uk 44). Siku nyingine jeshi hili likaingia kwa Chifu Ngata aliyepinga oparesheni yao. Alipigishwa magoti chini, wakamdunga visu mwilini na baada ya hilo, likawanajisi mabinti zake (uk 48).

Vijana wanatumia nguvu walizonazo dhidi ya wanawake wazee na dhaifu na kuwanajisi. Mambo alikuwa ni kijana mdogo sana wa jirani yake Mama Boke na aliyekuwa na umri sawa na wa Mwita mwanawe. Huyu ndiye aliyeshika hatamu ya mwisho katika kumnajisi mamake Mwita wakati jeshi lao lilipoingia. Hata alimwonya Boke asijaribu kwenda hospitalini huku akimtomasa kwa kidole chake (uk 107).

Vijana wanatumiwa vibaya na matajiri. Wanatumiwa katika kuendeleza machafuko ya kikabila ambayo mwishowe yanawanufaisha watu matajiri. Meja-K ni kiongozi wa jeshi la vijana. Aliamka asubuhi moja ili kupokea msaada wa chakula na silaha zilizoletwa kwa ndege ya helikopta na wahisani na wafadhili. Silaha hizo zilitumika katika kutekeleza maafa kwa makabila ambayo hayakukubaliwa katika maeneo fulani fulani

Asilimia kubwa ya vijana wanaokaa bila kuwa na lolote la kufanya mwishowe wanajiingiza katika matumizi ya pombe haramu. Wengine wanazunguka ovyo ovyo mabarabarani na kuishia katika makundi yanayoharamishwa kwa imani kuwa watafaidika. Hili linadhihirishwa na mwandishi pale anapowataja wale vijana waliokwenda Dunga, Tendoni na Serega na baada ya kukosa kazi huko, walirudi nyumbani na wakajiunga na jeshi haramu la vijana (uk 54).

Baadhi ya vijana wanalipwa ili kutekeleza maovu. Uchochole na umaskini mkubwa unaoletwa na ukosefu wa ajira unawafanya vijana kutenda lolote mradi wapate mahitaji yao. Tunaelezwa na mtunzi kuwa siku moja Meja-K akiwa katika kambi ya jeshi la vijana, aliwaza kuhusu yale malipo ya vijana ya kila jumamosi. Aliona kuwa yalikuwa yamecheleweshwa wiki hiyo na asingependa yacheleweshwe tena. Aliwaza kuwa kama yangeendelea kucheleweshwa, ingekuwa vigumu kudhibiti imani ya vijana katika jeshi la vijana (uk 25). Vijana walikuwa ni hazina kubwa ya wanasiasa. Kwamba mwanasiasa yeyote ambaye angetaka vijana wa kuvuruga mikutano, walikuwepo tayari kunadiwa kwa pesa kidogo na ulevi (uk 70). Vijana wanaitwa katika mikutano ya usiku ili kupanga mikakati ya mashambulizi. Vijana katika jamii wanasawiriwa kama watu waliotayari kutenda lolote mradi walipwe, hata kama ni tendo baya. Hili latokana na sababu kuwa wao ni wahitaji kwa kule kukosa ajira. Watatenda maovu endapo watapata masilahi yao ambayo wanayakosa katika maisha.

Vijana ni watumizi na wasambazaji wakuu wa madawa ya kulevya. Wamesawiriwa na mtunzi kama watu walioghilibiwa na kuingia katika kina kirefu cha mihadarati. Wamo katika mitandao mikubwa sana ya kiulimwengu. Wanauza dawa kama vile hashishi ambazo zinawaletea pesa kubwa. Pesa nyingi wanazopata zinawatia wehu. Wanafanya la kufanya wakaacha la kuacha. Wanaamka mapema na kuzungusha dawa za kulevya katika kila maeneo. Wanafanya hivyo kwa kuwahonga polisi. Kazi hizo wanazifanya kwa zamu ambapo kila mmoja huhakikisha zamu yake ya kuzungusha dawa imeshughulikiwa vya kutosha (uk 73).

Kutokana na machungu na adha wanazopitia katika maisha, vijana hawapotezi nafasi yoyote ile wanayoipata katika kutekeleza maovu ya kisasi kwa ubaya, maonevu, dhuluma, ukatili au unyanyasaji wanaofanyiwa na jamii. Kiunzi chetu cha tatu cha Uhalisia Hakiki hudai kuwa mambo yanayotendeka katika jamii hayatendeki tu bila

kusababishwa na chochote. Tukio au matukio kama haya lazima yamesababishwa na jambo fulani. Hali mbaya ya maisha ndiyo inayowapelekea kutekeleza maovu ya kujilipizia kisasi.

Meja-K anamlipizia kisasi baba yake Mzee Makoti baada ya wao kunyang'anywa shamba lao na Chifu aliyesema kuwa Mzee Makoti hakustahili shamba hilo na likapewa tajiri mmoja kutoka Dunga. Meja-K na mamake waliahidiwa fidia la shamba hilo lakini kote mamake Meja-K alikokwenda kuomba msaada, hukupata usaidizi wowote.

Eddah alipokimbilia usalama wake kutokana na jeshi la vijana, ndipo aliposhikwa na kundi fulani la askari hao. Alipelekwa msituni ambapo kazi yake ilikuwa ni kuwapikia, kuwafulia na kutoa huduma za mapenzi kwa askari. Anakumbuka alipotoroka jinsi alivyolala katika miamba na mahandaki na siku nyingi akilala maporini. Hili lilimfanya aape kuwa angelipiza kisasi siku moja. Namna ya kulipiza kisasi hicho hakujua lakini aliapa lazima atakuja kulipiza kisasi pindi tu akipata fursa (uk 23-24).

Vijana wanachukulia hali ya kujilipizia kisasi kama ni haki yao. Hata mbele ya sheria kama vile mahakama, wana misimamo mikali ya kutaka kulipiza kisasi kwa maovu wanayotendewa na jamii. Kwa mfano katika mahakama alikopelekwa Mwita, Mali ya Mungu alishuhudia nduguye alivyorushwa nje ya mahakama na kutiwa katika lori la polisi. Mamake naye alilia kwa nguvu zake zote kumwona mwanawe alivyotendewa hali wakijua kuwa yeye hakuwa mhalifu kwa vyovyote. Mwandishi anasema kuwa Mali ya Mungu alitaka kulipiza kisasi kwa niaba ya nduguye lakini hakujua ni vipi. Alisimama hapo nje ya mahakama huku akiwa amekunja ngumi lakini wapi! (uk 90).

Wao ni wakatili na hawana huruma kamwe. Nchi Kavu alimgonga chifu Ngata kwa chuma alichokuwa nacho mkononi na kumfanya mkono kufa ganzi. Baadaye walimdunga visu mwili mzima huku familia yake ikishuhudia. Chifu Ngata alilia kwa uchungu mkali huku akiwaomba msamaha vijana aliowalea lakini hawakumsikiliza. Waliishia baadaye kumkata ulimi kinywani na kisha kumwua kama paa wa mwituni. Wanawatia watu wanaowashambulia makovu ya maisha kwa huo ukatili wao kama vile Eddah alivyofanywa. Hakuwa na masikio kwani yalikuwa

yamekatwa na jeshi la vijana. Hata wanawake waliovamiwa walielezwa na jeshi hilo kuwa wasijaribu kwenda hospitalini (uk 61 na 106).

## 5. 5 Hitimisho

Sura hii imebainisha na kufafanua nafasi ya vijana katika riwaya ya *Kovu Moyoni*. Aidha sura hii imehusika katika kudhihirisha uwezo na nguvu walizonazo vijana na ambazo zikiimarishwa zitakuwa msingi muhimu katika jamii.

Baadhi ya nafasi chanya kwa vijana ni pamoja na ari yao ya kujikomboa kiuchumi na uzalendo mkubwa walionao juu ya mataifa yao.

Nafasi hasi zilizodhihirika ni pamoja na maovu hasa ukosefu wa maadili kama unajisi ambalo ni suala lililotawala sehemu kubwa sana kwenye riwaya inayohusika. Aidha vijana wanaendeleza machafuko ya kikabila, matumizi ya pombe haramu pamoja na matumizi ya madawa ya kulevya.

# SURA YA SITA

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6 . 1 Utangulizi

Utafiti huu ulilenga kuchunguza nafasi ya vijana katika riwaya za Habwe: *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni* (2014). Tuliongozwa na nadharia ya Uhalisia Hakiki ambapo tulijikita katika kiunzi chake cha tatu. Hiki kinadai kwamba matukio au mambo yanayotendeka katika jamii hayatendeki tu vivi hivi bila kusababishwa na chochote. Kwamba lazima matukio yawe yameanzishwa au kusababishwa na jambo fulani. Hivyo basi hali wanazojipata vijana wanajipata humo kutokana na msukumo na maswala fulani fulani katika jamii.

## 6. 2 Muhtasari wa matokeo ya utafiti

Nafasi ya vijana katika *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni* ni mambo yanayojitokeza wazi. Msanii amedhihirisha nafasi yao katika jamii iliyojaa maovu ya ubinafsi, ufisadi na utabaka uliokithiri. Ameonyesha namna jamii ya aina hii inavyowatumia vijana kama watu wanyonge kujinufaisha kwa kuongozwa na huo ubinafsi.

Katika utafiti wenyewe tulikuwa na madhumuni matatu. Kwanza kabisa tulilenga kuchunguza changamoto zinazowakabili vijana katika riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni*. Hili tulilitekeleza kwa njia ya kutathmini hali na maisha ya jamii kwenye riwaya hizo mbili. Pili tulibainisha na kufafanua nafasi ya vijana katika riwaya zetu kama zilivyodhihirishwa na msanii katika kazi zake. Tuliainisha nafasi ya vijana kuwili: nafasi chukivu au hasi na vile vile nafasi chanya. Matokeo ya utafiti wetu yamedhihirisha kuwa, vijana wanachukua nafasi hasi au chukivu sio kwa mapenzi yao ila ni kutokana na hali ya maisha ya jamii na changamoto wanazokumbana nazo. Kwa mfano, vijana hawasikilizi wazazi wao. Hawaoni baadhi ya mawaidha wanayopewa na wakuu wao kama ya manufaa kwao ila ya kuwavuta nyuma wakati wao wanataka kujiendeleza na kujitoa katika matatizo yao. John Habwe amefaulu kuisawiri hali hii kwa kutumia wahusika kama vile Rukia, Kudra na Regina katika *Pendo la Karaha*, Eddah na Mali ya Mungu kwenye *Kovu Moyoni*.

Imejitokeza pia kuwa maadili yamewapotoka vijana kwa kiasi kikubwa. Eddah ana bakwa mbele ya mamake na jeshi la vijana katika *Kovu Moyoni* wakati ambapo Lindo anacheza bao na mzee wa rika na babake, mzee Mwamba. Wengine wanapigwa picha wakiwa uchi na watalii kwenye *Pendo la Karaha*. Mwandishi huyu ametuchorea picha halisi kama ilivyo katika jamii nyingi za kiafrika.

Imedhihirika vile vile kuwa vijana wanatumiwa kwa kukandamizwa na waajiri katika sehemu zao za kazi pamoja na kudhulumiwa kimapenzi. Wengine wakishirikishwa katika vita vya kikabila katika jamii na viongozi mbalimbali. Vijana wamechorwa kama wanaovumilia changamoto hizi katika juhudi zao za kutafuta riziki na mustakabali wao.

Kutokana na madhila wanayopitia vijana kwenye jamii, imedhihirika kuwa ni watu wanaotenda maovu ya kujililipizia kisasi pale wanapotendewa udhalimu. Mwandishi amewatumia wahusika kama vile Meja-K, Eddah, Mali ya Mungu na Sela kwenye *Kovu Moyoni*, Kudra na Teresa Almasi katika *Pendo la Karaha*. Baadhi yao wanalipiza kisasi hicho, wengine wanakosa uwezo huo kutokana na udhaifu au unyonge walionao. Mwandishi wa riwaya hizi amedhihirisha hali hii na kuonyesha kuwa haya wayatendayo sio kwa kupenda kwao ila ni msukumo unaotokana na hali ya maisha katika mazingira yao.

Matokeo ya utafiti wetu yamebainisha kuwa vijana wanaochochewa kwa urahisi na hasa katika kutenda mambo yasiyostahili. Viongozi wenye ubinafsi katika jamii wanawachochea vijana wanaoingia katika maovu huku wakijinufaisha wao. Wanawatumia vijana kwa kuongozwa na huo ubinafsi ili waendelee kubakia katika mamlaka na utawala. Wengine wanadanganyika na kuingizwa katika ulanguzi wa dawa za kulevya kama ilivyojitokeza katika riwaya zetu za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni*.

Usambazaji wa dawa za kulevya pamoja na matumizi yake ni shughuli ambayo imedhihirika kutekelezwa na vijana katika jamii. Msanii amedhihirisha hali hii na kuonyesha kuwa vijana wanapewa kazi hii ya usambazaji dawa na watu wenye uwezo wa kiuchumi kwa mshahara ambao mara nyingi ni zizo hizo dawa kwa matumizi yao wenyewe.

Matokeo ya utafiti wetu yamedhihirisha vile vile kuwa vijana wetu katika jamii ndio wanaoshirikishwa katika mapigano au vita vya kikabila. Hili linatokea sana katika mataifa mengi yanayoendelea. Vijana wanatokea kutumika kwa urahisi kwa sababu wao ndio wanaopatikana vile vile kwa urahisi. Sababu kuu hapa ni kwa kuwa asilimia kubwa ya vijana wetu haina ajira na kwa hiyo wanaonekana kukaa bila ya kujishughulisha na lolote. Viongozi nao wanachukuwa nafasi hiyo na kuwaahidi pesa ili watekeleze maovu ya mashambulizi katika riwaya ya *Kovu Moyoni*.

Katika kuangazia hali hizi, msanii ameonekana kuzielewa vilivyo nafasi hasi na chukivu wanazopewa vijana katika jamii. Kwa maoni yetu, mwandishi huyu amefaulu amebainisha nafasi hasi na chanzo chake hasa baada ya kutuchorea picha halisi ya maisha yalivyo kwenye jamii katika riwaya zilizohusika.

Licha ya nafasi hasi na chukivu, John Habwe amefaulu katika kuwajenga na kuwatambulisha vijana na mchango wao muhimu. Anaizindua jamii ili iweze kutambua umuhimu huu na kuutilia maanani katika kuijenga jamii. Ameangazia bidii ya vijana katika juhudi za kujikomboa kutokana na umaskini. Amewatumia wahusika kama vile Kudra na Rukia kwenye *Pendo la Karaha,* Eddah na Mali ya Mungu katika *Kovu Moyoni.*

Imedhihirika kuwa vijana ni watu wenye misimamo imara dhidi ya vitendo visivyostahili kwenye jamii. Hili linawajenga kimaadili kwani wanaonekana kuwa ange na macho wakati wanaletewa majaribu ya kufanya mambo yasiyofaa. Kudra alikataa kabisa kutumiwa kimapenzi na mwajiri wake hata baada ya vitisho vyake, hali tunayoiona katika *Pendo la Karaha*. Mali ya Mungu alikataa katakata kushawishiwa na Yoko pamoja na Situma kuingia katika biashara ya dawa za kulevya katika *Kovu Moyoni*. Aidha Mwita naye alikuwa imara mahakamani alipomtaka hakimu mwenyewe amfunge badala ya maswali ambayo yeye mwenyewe hakimu alijua wazi hayangemwokoa. Hili lilidhihirika katika riwaya ya *Kovu Moyoni*

Utafiti huu umedhihirisha kuwa vijana ni wenye kuwajibikia na kuwatunza wazazi wao. Wanawaonea imani na huruma kubwa wanapowaona wazazi wao wakiteseka wanapowashughulikia. Katika *Pendo la Karaha*, Kudra alitoka shule ili kumwondolea mamake kero la kulipa karo na vitabu vya bei ghali. Alimtaka mamake aiache

biashara aliyokuwa akiifanya alipogunduwa mamake alikuwa akiugua. Eddah katika *Kovu Moyoni* alijishughulisha katika kazi nyingi bila kuchoka zikiwemo upishi wa maandazi ili amsaidie mamake mjane.

Matokeo mengine ya utafiti huu yamebainisha wazi kuwa vijana ni mihimili muhimu sana katika jamii. Mashirika ya kuwashughulikia vijana katika masuala ya kazi, elimu, mapenzi na hatari ya dawa za kulevya yanatumiwa katika kuwaleta vijana pamoja na kujadili changamoto zinazotokana na ulevi huu. Mashirika haya yanawathamini vijana kwa kuutambua umuhimu wao katika mataifa yao.

Mbali na nafasi ya vijana katika riwaya husika, tulizichunguza changamoto zinazo wakumba vijana. Shughuli hii tuliitekeleza katika sura ya pili kwenye *Pendo la Karaha* na katika sura ya nne kwenye *Kovu Moyoni*. Changamoto zilizoibuka ni pamoja na ukosefu wa ajira katika mataifa mengi, suala linalotishia uhai wa kizazi kizima cha vijana. Umaskini, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya, dhuluma za waajiri kazini pamoja na kudhulumiwa kimapenzi, unafiki wa viongozi walio mamlakani pamoja na mashambulizi ya kikabila yanayochochewa na viongozi wanaojitakia makuu ni baadhi ya changamoto wanazopambana nazo vijana katika jamii.

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya Uhalisia Hakiki ambapo riwaya inayohusika imelengwa kuihakiki jamii. Ni kutokana na mwongozo wa nadharia hii uliotuelekeza katika kuitathmini jamii mwanzo katika riwaya tulizoshughulikia za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni* za John Habwe. Hili lilitupa picha kamili ya hali ya maisha ya jamii kwenye riwaya zote husika. Kwa hiyo utafiti wetu umedhihirisha sababu na chanzo cha vijana kujipata katika hali walizomo au kuchukua aina ya nafasi wanazochukua, hasi na chanya.

Uwasilishanji wa maudhui ya nafasi ya vijana katika riwaya zinazohusika umefaulu kwa kiasi kikubwa. Tumeifikia kauli hii kwanza kwa kuwa mwandishi amewalenga vijana kwani ndio ambao wamekuwa ni wahusika wakuu katika kazi zake zilizohusika. Pili ni kwamba mwandishi amejikita sana katika maswala yanayowahusu vijana kama vile ukosefu wa ajira, matumizi ya dawa za kulevya na ukosefu wa maadili katika kutaja machache. Amewakweza vijana kwa nafasi chanya

kama vile kuwa ni mihimili ya taifa, wanaowajibikia wazazi wao na wenye ari ya kujikomboa kiuchumi katika kutaja machache

### 6.3 Changamoto za utafiti

Kwa kuwa sampuli tulioteuwa ilikuwa ni sampuli lengwa, kazi yetu ilikuwa na changamoto mbili kuu. Kwanza tulimlenga mwandishi mmoja, John Habwe. Mbali na riwaya zilizohusika katika utafiti wetu, ilitubidi tusome riwaya nyingine alizoandika nazo zilikuwa nyingi. Hili halikuwa ni jambo rahisi kwa kuwa mwandishi huyu ameandika riwaya nyingi.

Changamoto nyingine ilitokana na kwamba nadharia ya uhalisia hakiki haijatokea kuandikiwa kwa kina kwa lugha ya Kiswahili. Ilitulazimu kuchukua muda wetu katika kusoma maelezo yake kwa kiingereza na kutafsiri maelezo hayo. Licha ya changamoto hizo tuliweza kufaulu katika kukusanya data zilizotufaa.

### 6.4 Hitimisho

Imejitokeza kuwa changamoto ziwakumbazo vijana katika jamii yetu ndizo zinazowapelekea vijana kuchuwa nafasi mbalimbali katika jamii hiyo. Vijana wamechukua nafasi chanya na hasi kutokana na msukumo unotokana na jamii wanamokulia. Tumefikia kauli hii kwa kuongozwa na kiunzi cha tatu cha nadharia ya uhalisia hakiki kwamba matokeo yoyote huwa yameanzishwa na mambo fulani. Kwa hiyo vijana wanapochukua nafasi hasi, hawafanyi hivyo kwa mapenzi yao ila ni huo msukumo unaotoka katika hali ya maisha ya jamii wanamokulia.

### 6. 5 Mapendekezo

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya Uhalisia Hakiki yenye viunzi vitatu kulingana na Collier, (1994:42-45). Sisi tulijikita katika kiunzi cha tatu kinachodai kwamba matukio au mambo yanayotendeka katika jamii hayatendeki tu vivi hivi bila kusababishwa na chochote, lazima matukio yawe yameanzishwa au kusababishwa na jambo fulani.

Pendekezo letu ni kuwa tafiti za baadaye ziweze kuangazia mada yenyewe kwa kujikita katika Viunzi Vingine vya nadharia ii hii ya Uhalisia Hakiki.

Utafiti pia unaweza kufanywa kwa kuongozwa na nadharia nyingine.

## MAREJELEO


Acher, M. et al. (1998). *Critical Realism: Essential Readings.*London: Routledge.

Becker, Eva (2011) `Youth Rights in The Kenyan Constituition.' Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Uppsala Sweden. (Haijachapishwa).

Bhaskar, R.A (1998). *The Possibility of Naturalism: A Physical Critique of the Human Science.*London: Routledge.

Collier, A. (1994). *Critical Realism: An Introduction to Roy Bhaskar's Philosophy*, London: Verso.

Erikson, H.E. (1961*). Youth Change and Challenge*. New York: America Academy of Art and Science.

Government Printers (2010). *Katiba Ya Jamhuri Ya Kenya.* Nairobi: International Institute for Legislative Affairs

Habwe, J. (2014). *Pendo la Karaha*. Nairobi: Moran East African Educational Publishers Ltd.

____________(2014). *Kovu Moyoni*.Nairobi: Bookmark African Publishers.

___________ (2014*). Hadaa Ya Nafsi*.Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

____________(2011*). Safari Ya Lamu*. Nairobi: Longhorn Publishers

Kingei, K na Kobia, J. (2007). *Lugha kama Kitambulisho: Changamoto ya Sheng Nchini Kenya.*Nordic Journal of African Studies 16(3):320-332 Kenya.

Kiongera, K. J. (2012). Mchango wa Vijana katika kuleta Mabadiliko Chanya Katika Tamthilia Teule za Kiswahili. Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kipyegon, K. (2013). Nafasi na utambulisho wa mwanamke katika Natala na Kifo Kisimani. Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa)

Katola, E. (2006). Udhalimu Dhidi ya Wahusika wa Kike Katika Tamthilia za Kiswahili. Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kruger (1998). *Female Characters in Contemporary Kenya Women Writers;* Figures of subdued London: Longhorn.

Lugano, R. (1989). Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi. Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Masibo, B. (2009). Gendered Perspective in the Novels of Ngugi wa Thiong'o and Alice Walker. Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi.*Nairobi: Standard Text Books Graphics and Publishing

Mugenda, O. & Mugenda, G. (1999). *Research Methods. Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Acts Press.

Mirikau, S.A. (2011). Taswira ya Mwanamke Katika Tamthilia za K.W. Wamitila.Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapiswa).

Millet, K. (1969). *Sexual Politics*. New York: Doubleday and Company Ic.

Mogambi, K. (1983). 'Hali ya Wanyonge kama Inavyojitokeza katika Riwaya za S. Mohammed.'Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Murono, S.E. (2005). Tadubiri za insha. Dar-es-salaam: Longhorn Publishers.

Mutua, J.M. (2007). 'Mitazamo ya Vijana na Wazee Kuhusu Ukombozi wa Wanawake'Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Naliaka, E.K. (2013). Uhakiki wa Hali ya Vijana Katika Riwaya ya Vipanya vya Maabara: Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Njogu, K. na Chimera R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*: *Natharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nyamemba (2013). Uchanganuzi linganishi wa maswala ya vijana na jinsi yanavyoshughulikiwa na waandishi katika diwani ya Tunu ya Ushairi: Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Obore, E.M. (2012) Dhuluma Dhidi ya Vijana wa Kike katika Riwaya ya Rosa Mistika. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Pawson, R. and Tilley, N. (2002). *Realistic Evaluation*. London: SAGE Publications Ltd.

Sayer, A. (1994). *Critical Realism: An introduction to the Philosophy of Roy Bhaskar*, Verso, London.

Sayer, A. (1999). *Realism and Social Science,* SAGE, London.

Senkoro, F.E.M.K (1982). *Fasihi*. Dar-es Salaam: Press and Publicity Centre.

*U.N World Youth Population Monitoring, Adolescence and youth*: Aconcise Report, New York 2012.

Wafula, R.M na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

____________ (2002 a). *Kichocheo cha Fasihi*: *Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

___________(2003b). *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

___________(2008). *Kanzi ya Fasihi 1*: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wanjiku, K na Akinyi, N (1993). *Celebrating Womens resistance. A case study of Women Groups Movement in Kenya*. Nairobi: Africa Women Perspective.

Weller, R. & Austin, W. (1986). *Theory of literature*. London: Harcourt.

*Youth Challenge International Annual Report*, Secretary-General`s Report to the General Assembly, A/36/215, 1981.